

**MANDONGA KUFUNGA MWAKA NA NGUMI YA 'CHIFU KINGALU'**
UKURASA 23

**PAPA** atangaza Mafinga Jimbo, amteua Askofu
UKURASA 2

**OFISA** elimu, mhandisi jiji matatani kwa ujenzi wa shule
UKURASA 15



**UCHAGUZI DRC:** Matokeo kura urais kuanza kutangazwa
UKURASA 17


# Nipashe

Jumamosi Desemba 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581533

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


## UTAFITI WABAINI:

# Pombe, sigara chanzo maradhi ya moyo Watoto



**IWAPO** mama atakunywa, kuvuta wakati wa ujauzito...

*Endelea ukurasa 3*

## CHADEMA yalia maridhiano kutotekelezwa



UKURASA 2

## Serikali yaibua kliniki ya ardhi kiganjani katika utatuzi migogoro

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA NA YANGA MAJARIBUNI BARA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Katibu Mkuu wa Chadema John Mnyika akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho Kinondoni jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kulalamikia barua ya miswada ya sheria ya uchaguzi aliyoiandika mwezi Julai kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa haijajibiwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CHADEMA yalia maridhiano kutotekelezwa

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimedai kuwa kuna mambo makubwa ambayo hayajafanyiwa kazi katika maridhiano ikiwamo mchakato wa Katiba Mpya.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu barua ya Julai 19, mwaka huu, ambayo chama hicho kilimwandikia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambayo amedai mpaka sasa hawajapata majibu yake.

Kuhusu maridhiano, Mnyika alisema baada ya kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan Mei, mwaka jana, kuna ajenda 11 ambazo waliziwasilisha kwake huku zilizofanyiwa kazi kati ya hizo ni sita tu.

"Kwenye mazungumzo tulipeleka agenda ya kuundwa kwa tume ya ukweli ya upatanishi na haki yenyewe haihusiani na mambo ya muswada, tulisema Rais aunde hii tume. Ajenda tulizopata maridhiano ni ya kuruhusu mikutano.

"Katika ajenda sita, ziko mbili ambazo ni muhimu kwa serikali kupeleka muswada wa kuendeleza mchakato wa Katiba Mpya na suala hili halijafikiwa maridhiano," alisema.

Mnyika alisema kama kuna dhamira ya kweli ya maridhiano, wangepeleka bungeni muswada wa Katiba. Huku akidai kuwa kuna dalili Katiba isipatikane hadi wanapofikia uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Jambo hili CCM (Chama Cha Mapinduzi) hawalitaki. Je, wanaweza kuwa na ujasiri wa kutoka hadharani kueleza kuwa CHADEMA wamepewa kila kitu wakati kuna mambo makubwa ya maslahi ya umma hayajafanyiwa kazi.

"Maridhiano hayajapatikana yote kuwapo kwa mkutano wa hadhara hakuna marekebisho ya Katiba ili tupate uchaguzi wa haki. Hakuna maridhiano katika mambo ya msingi ambayo tuliyawasilisha," alisema Mnyika.

Kuhusu barua kwa Waziri Mkuu, Mnyika alisema wanamwomba kujitokeza na kutoa majibu kuhusiana na miswada ya sheria ya uchaguzi na sheria ya vyama vya siasa.

"Tuliamini Ofisi ya Waziri Mkuu itatoa majibu ya muafaka. Julai 19, mwaka huu, nilimwandikia barua Waziri Mkuu Majaliwa yenye kichwa cha habari, 'Mchakato wa Katiba Mpya na marekebisho ya Katiba kuwezesha uchaguzi huru na haki'," alisema.

Mnyika alisema tangu alipowasilisha barua hiyo, hadi sasa hakuna majibu kinyume cha mwongozo na taratibu zinazoongoza Ofisi ya Waziri Mkuu. Alisema baada ya kukosa majibu, Septemba, mwaka huu, alikwenda Ofisi ya Waziri Mkuu lakini hakumpata.

Alisema waliwasilisha mapendekezo na marekebisho ya Katiba kwa namna gani ipatikane ili kuwezesha uchaguzi kuwa huru na haki na walitakiwa kufanya hivyo kabla ya kuwasilisha muswada bungeni.

Alisema mapendekezo ya wadau kabla ya muswada kupelekwa bungeni hawakujulishwa ili kuyajadili na kuboreshwa mapema.

"Hakuna hatua zozote zilizochukuliwa ikiwamo kuwashirikisha wadau matokeo yake wakapeleka moja kwa moja miswada mibovu na mibaya bungeni Novemba 10 mwaka huu," alidai Mnyika.

Alisema kwa kuwa barua hiyo haijajibiwa licha ya jitihada mbalimbali walizozifanya, chama chao kinamuomba Waziri Mkuu au Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, kuyatoa kwa kuwa jambo hilo la muswada linawahusu.

"Tatizo likiwa kwenye katiba ukipeleka muswada wa sheria ikiwa huo muswada haujagusa katiba hata upokee maoni namna gani Kamati ya Bunge haiwezi kupeleka marekebisho.

Mnyika alisema jambo linalogusa katiba kuna mambo mawili ya kuzingatiwa ambayo ni kuwapo katiba mpya au kuirekebisha.

Mnyika alisema miswada yote mitatu iliyopelekwa bungeni haihusu uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Alisema serikali inakusudia uchaguzi huo kuendeshwa kwa mfumo ule wa kusimamiwa na Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa kupitia kanuni zinazotungwa na waziri husika na kueleza hizo ndio kanuni.

"Taifa likikubali tukapitia njia hiyo uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani zitakuwa za hovyo kama za mwaka 2019. Rai yangu Watanzania wote na wadau wa demokrasia kwa pamoja watake mabadiliko ya sheria za uchaguzi wa serikali za mitaa," alisisitiza.

## Papa atangaza Mafinga jimbo, amteua Askofu

**Na Romana Mallya**

BABA Mtakatifu Fransisko, ametangaza Jimbo jipya la Kanisa Katoliki la Mafinga mkoani Iringa na kumteua Padri Vincent Mwagala kuwa Askofu wa kwanza.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, uteuzi huo ulianza jana. Kabla ya kuwa jimbo, Mufindi ilikuwa sehemu ya Jimbo la Iringa.

Alisema Mhashamu Askofu Mteule Mwagala alizaliwa Desemba 11, 1973 kijiji cha Makungu, Mufindi, Jimbo la Katoliki Iringa.

"Baada ya masomo na mafunzo ya kipadri, alipewa daraja takatifu la Upadri Julai 11, 2007 jimboni Iringa na kuhudumu katika nafasi mbalimbali za utume nchini Italia na Iringa," alisema Dk. Kitima katika taarifa hiyo.

Dk. Kitima alisema Mwagala aliteuliwa kuwa Makamu wa Askofu mwaka 2018 na mwaka 2019 aliteuliwa kwenye Baraza la Washauri wa Askofu Jimbo la Iringa hadi alipoteuliwa kuwa Askofu wa Jimbo la Mafinga.

"Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania linamwombea Mhashamu Askofu Mteule Mwangala afya ya roho na mwili katika utume huo mpya jimboni Mafinga," ilisema taarifa hiyo.

# Polisi yajipanga kukabili uhalifu Krismasi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limesema limeweka mikakati ya kukabiliana na uhalifu wa aina zote wakati wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya huku likiwaonya wale watakaojihusisha na vitendo hivyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, miongoni mwa mikakati ni kutoa elimu ya kuzuia uhalifu.

Alisema mikakati mingine ni kufanya misako na operesheni za kuwakamata wale wote watakaovunja sheria kwa kutenda uhalifu wa kijinai au kuvunja sheria za usalama barabarani.

"Tunaendeleza mikakati ya kutoa elimu ya kuzuia uhalifu, kufanya misako na operesheni za kuwakamata wale wote watakaovunja sheria kwa kutenda uhalifu wa kijinai au kuvunja sheria za usalama wa barabarani," alisema.

Misime aliwataka wazazi na walezi katika msimu huu wa sikukuu kutowaruhusu watoto wao kwenda kwenye maeneo ya mikusanyiko inayoruhusiwa, bila kuwa na mtu wa kuwalinda au kuwaongoza.

Alisema licha ya Jeshi la Polisi kujipanga vizuri, linaendelea kutoa wito kwa wananchi kutambua kuwa usalama unaanza na mtu mwenyewe, hivyo wahakikishe nyumba zao haziachwi bila uangalizi.

Pia aliwataka watumiaji wa barabara kuepuka vitendo hatarishi kama vile kuendesha vyombo vya moto kwa mwendokasi, wakiwa katika hali ya ulevi, kupita magari mengine bila tahadhari hasa katika kona na mwinuko.

"Tunataka wananchi waepuke kuchoma matairi barabarani, kupasua chupa na kuleta vurugu badala ya kusherehekea na kushangilia kwa amani.," alisema.

RPC TANGA AONYA

Mkoani Tanga, Jeshi la Polisi limewataka wananchi kusherehekea Krismasi na Mwaka Mpya kwa amani na utulivu bila kujihusisha na vitendo vya uhalifu au vyenye kuashiria uvunjifu wa sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa Tanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Almachius Mchunguzi, alisema jana kuwa vyema wananchi wakachukua tahadhari kwa kushirikiana na jeshi hilo kuhakikisha vitendo vyote vya uhalifu na wahalifu katika maeneo mbalimbali vinadhibitiwa endapo vitajitokeza.

Kamanda Mchunguzi amesema jeshi la polisi limejipanga kikamilifu kuhakikisha wananchi wote wanasherehekea sikukuu kwa amani na utulivu kutokana na kuimarishwa kwa ulinzi katika ya nyuumba za ibada, starehe na burudani na maeneo yote ya wazi yatakayokuwa na mikusanyiko ya watu.

Aliwataka pia amewataka wamiliki wa kumbi za starehe kuzingatia uhalali wa matumizi katika uingizaji watu, umri unaostahili na zaidi kujali uwezo wa ukumbi huku akipiga marufuku disko toto.

Pia aliwataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuendelea kuwa makini zaidi na uangalizi wa watoto wao, wa majirani na watoto wa jamii kwa ujumla waepuke kuwaacha wakitembea peke yao au kuzurura barabarani na maeneo mengine ili kuepuka ajali na maafa au matukio mengine.

Aidha, alitoa onyo kwa wazazi kuwa ni marufuku watoto kwenda ufukweni mwa bahari peke yao na kwamba mtoto atakayepata matatizo ya kupoteza maisha kwa sababu ya kuogelea, mzazi atachukuliwa hatua za kisheria.

## HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na mgeni wake Balozi wa India Nchini Tanzania Binaya Srikanta Pradhan (kulia) alipofika Ikulu Jijini Zanzibar kwa mazungumzo na kuaga, baada ya kumaliza muda wake wa kazi nchini, mazungumzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Pombe, sigara chanzo magonjwa moyo watoto

**Na Raymond Mtani,** BMH

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kwa Watoto katika Hospitali ya Rufani ya kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), Victor Urio, amesema pombe na sigara ni miongoni mwa vyanzo vinavyoweza kusababisha watoto kuzaliwa na magonjwa yakiwamo ya moyo.

Dk. Urio aliyasema hayo jana kuwa huku akibainisha kuwa utafiti unaonyesha kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa hai kote duniani, wanane huwa na hitilafu mbalimbali za moyo.

Pia alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kuwa zaidi ya watoto 240,000 hufariki dunia kwa magonjwa ya kuzaliwa nayo yakiwamo ya moyo kila mwaka kabla ya kufikisha siku 28.

Vilevile alisema kwa mujibu wa WHO, zaidi ya 170,000 hufariki dunia wakiwa na umri kati ya mwezi mmoja na miaka mitano kwa magonjwa hayo.

"WHO inatanabaisha watoto tisa kati ya 10 wenye magonjwa ya kuzaliwa nayo, wanatoka nchi za zenye uchumi wa chini na wa kati, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zikiwa miongoni," alisema.

Dk. Urio alisema takwimu hizo hazitofautiani na zinazoonekana katika kliniki ya watoto ya Hospitali ya Benjamin Mkapa.

"Kila mwezi tunaona watoto kati ya 10 hadi 20 wakiwa na magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo," alisema Dk. Urio.

Alisema kama ilivyo duniani kote, matundu na mishipa ambayo haijafunga kwenye moyo ni miongoni mwa hitilafu zinazowakabili watoto wengi wanaobainika kuwa na magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo hospitalini hapo.

"Ingawa wataalamu hawajabaini sababu halisi za watoto kuzaliwa wakiwa na hitilafu kwenye moyo, yako mazingira yanayoongeza uwezekano wa mama kujifungua mtoto mwenye hitilafu za moyo.

"Kutumia pombe na kuvuta sigara wakati wa ujauzito ni tabia zinaongeza uwezekano wa mama kujifungua mtoto mwenye hitilafu katika moyo," alibainisha.

Dk. Urio alitaja sababu nyingine ya mjamzito kujifungua mtoto mwenye hitilafu ya moyo ni kitendo cha kuchelewa kuanza kliniki na kuchelewa kuanza matumizi ya vidonge vyenye madini ya foliki.

"Vile vidonge vya foliki vinahusika katika kujenga maumbile ya mtoto. Lakini ziko sababu za kurithi na za kimaumbile na wakati mwingine maambukizi anayoyapata mama wakati wa ujauzito.

"Mfano virusi vya Rubella vinaweza kumweka katika hatari ya kujifungua mtoto mwenye hitilafu kwenye moyo," alisema.

Dk. Urio alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazopambana kuimarisha sekta ya afya kwa kasi kubwa kwa kuhakikisha huduma za afya zinapatikana jirani na mazingira wanayoishi wananchi wake.

Vilevile alisema serikali inapambana kuboresha utoaji wa huduma kwa kupeleka wataalamu na vifaa tiba na sasa kuleta bima ya afya kwa wote ambayo italeta unafuu wa gharama za matibabu.

# Serikali yaibua kliniki ardhi kiganjani utatuzi migogoro

**Na Joseph Mwendapole**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imezindua kiliniki ya ardhi kiganjani ambayo itawawezesha wananchi popote walipo kuwasilisha kero za ardhi na kupata suluhisho la matatizo kutoka kwa viongozi wa serikali.

Kadhalika, Wizara hiyo imeagiza kuanzishwa kwa kliniki za ardhi kwenye mikoa yote nchini ili kuwawezesha wananchi kupata suluhisho la matatizo ya ardhi papo hapo.

Uzinduzi wa kiliniki hiyo ulifanywa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Jerry Silaa, alipokutana na kufanya mazungumzo na waandishi wa habari na wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) kuzungumzia mafanikio ya siku 100 tangu ateuliwe na Rais Samia Suluhu Hassan, Agosti, mwaka huu.

Silaa alisema matatizo ya ardhi nchini ni makubwa na ndiyo sababu wizara inakusudia kuanzisha 'one stop land clinic' za ardhi kwenye mikoa yote kuanzia Januari, mwakani, ili kupunguza matatizo hayo. Alisema kiliniki hizo za wazi zitakuwa msaada mkubwa kutatua shida za wananchi wengi kwa muda mfupi na alitaka kiliniki hizo ziwe za wazi ili wananchi wote wasikie namna kero zinavyotatuliwa.

"Nataka muundo wa kliniki zote za ardhi zitakazofanyika nchi nzima zifanyike kwenye maeneo ya wazi kama mahema maana hakuna siri, tunataka mwananchi akifika akute maofisa wa serikali wanohusika wako sehemu moja ili kuondoa mianya ya rushwa na usumbufu wa nenda rudi," alisema.

"Makamishna wote wa ardhi nchini wanapaswa kuandaa ratiba ya kniliki za ardhi kusikiliza kero za wananchi ambazo zitawawezesha viongozi wa serikali kuwapo kwenye kliniki hizo, kama siyo mimi Waziri basi awepo Naibu Waziri au Katibu Mkuu wa Wizara ili wananchi wapate suluhisho la maatatizo yao hapo hapo.

"Nimesema hivyo kwa sababu kuna wananchi watakaokuja kwenye kliniki hizo walalamikiwa wakiwa maofisa ardhi watakaowakuta hapo. Sasa kama hawatawakuta viongozi wa wizara haitakuwa rahisi kwao kutendewa haki," alisema. Silaa alisema wizara itafanya maboresho ili ofisi zake zote ziwe na kamera zinazoonyesha watumishi waliofika ofisini wamefika muda gani ili kuondoa utamaduni wa watumishi kuzembea kwenye majukumu yao.

"Nataka ifike wakati kiongozi akija akiuliza watumishi wa ardhi wako wapi aweze kuwaona kwa sura na majina yao kupitia teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA). Hili likifanyika litaongeza uwajibikaji kwa watumishi wa sekta ya ardhi," alisema.

Kwa mujibu wa Silaa, wizara inajipanga kufanya maboresho makubwa ya sera, sheria na kanuni na kupitia sheria zote za ardhi za sasa ili kuzifanyia marekebisho na kupata sheria na kanuni zinazotoa majibu kwa matatizo ya ardhi yaliyopo kwa sasa.

Alisema kwenye maboresho hayo, wizara imejiwekea mkakati wa kuhakikisha maeneo yote nchini yanapimwa kwa kushirikiana na kampuni binafsi ambazo zitafanyiwa uhakiki na serikali.

Silaa alisema awali kulikuwa na kampuni nyingi za upimaji ardhi ambazo hazikukidhi vigezo zilizochukua fedha za wananchi na kushindwa kukamilisha kazi lakini Wizara imefanya mchujo na kuzifutia usajili.






Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Salum Khamis Rashid (kulia) akikabidhi msaada wa chakula katika kituo cha yatima cha Assalam Ophen Centre, ambao ulitolewa na Mamlaka ya Mafunzo na Amali juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kizimbani madai ya kumuua wifi yao

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

WATU wawili wanaotuhumiwa kuhusika na mauaji ya Flora Philemon, mkulima na mkazi wa Nyamohongolo Manispaa ya Ilemela wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza na kusomewa mashtaka ya mauaji.

Waliosomewa shtaka katika kesi namba 40349/2023 ni Elizabeth Ndakidemi (35) Mkazi wa Dar es Salaam ambaye pia ni wifi wa marehemu na Faida Masaba (24), mkazi wa Igoma, Nyamagana mkoani hapa.

Washtakiwa hao wote kwa pamoja wanadaiwa kushirikiana kumuua Flora Philemon kinyume na kifungu namba 196 na 197 ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022. Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Fortunatus Kubaja, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Monica Mweli, alisema washtakiwa walitenda kosa hilo Novemba 13,2023 eneo la Nyamhongoro, Ilemela mkoani Mwanza.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, washitakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka kisheria ya kusikiliza kesi hiyo na shauri hilo.

Baada ya kusikiliza maelezo hayo, Hakimu Kubaja aliahirisha shauri hilo hadi Januari 4, 2024.

Tukio hilo la mauaji liliripotiwa kutokea Novemba 14, mwaka huu, saa 11:00 jioni katika Mtaa wa Kashishi, Kata ya Nyamhongolo wilayani Ilemela. Ilidaiwak uwa Philemon aliuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili. Kwa mujibu wa jeshi la polisi, upelelezi na ufuatiliaji wa haraka na kuwakamata watu wawili, akiwamo wifi wa marehemu kwa kupanga na kuhusika na njama za mauaji hayo yanayodaiwa kutokana na migogoro ya kifamilia ya kuwania mali.

## 'Watumishi jipimeni na mifumo mtandao'

**Na Veronica Mwafisi,** DUMILA

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, amewataka watumishi wa umma katika Halmashauri Wilaya ya Kilosa, Kanda ya Dumila kujipima kupitia mifumo mipya ya PEPMIS, PIPMIS na HR Assessment.

Amesema wanatakiwa kujipima kwa kujaza kazi wanazotekeleza kila siku ili mfumo uweze kutoa alama sahihi.

Daudi alisema hayo jana alipotembelea kanda ya kimafunzo ya Dumila kuona maendeleo ya mafunzo ya mifumo hiyo.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwaongezea watumishi wa umma ujuzi na ari ya kutumia mifumo ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) katika kupima utendaji kazi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali serikalini.

"Serikali inafanya juhudi kubwa katika kusimamia na kutoa stahiki na maslahi mbalimbali kwa watumishi wa umma, hivyo ni jukumu la watumishi kuiunga mkono kwa kutoa huduma bora kwa umma," alisema Daudi.

Aliongeza kuwa moja ya majukumu ya Ofisi ya Rais -UTUMISHI ni kusimamia utumishi wa umma, ndiyo maana serikali imebuni mifumo hiyo ambayo itaboresha utendaji kazi serikalini kwa kumpima mtumishi mmoja mmoja na taasisi.

Daudi alifafanua kuwa kupitia mfumo wa PEPMIS, kila mwajiri atakuwa na uwezo wa kuona namna watumishi wake wanavyofanya kazi kila siku.

Naibu Katibu Mkuu alieleza kufurahishwa na watumishi wa umma katika mkoa wa Morogoro walivyoitikia wito wa kushiriki mafunzo hayo na wameonyesha utayari wa kutumia mifumo hiyo ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan anayetaka kuona kunakuwa na utumishi wa umma bora na wenye kuhudumia wananchi kwa ufanisi mkubwa.

# SUA yawezesha wakulima mafunzo akili bandia

**Na Romana Mallya**

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kimetoa mafunzo ya mfumo wa akili bandia kwa afya ya mimea kwa baadhi ya wakulima wa wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Mafunzo hayo yana lengo la kusaidia kufuatilia njia bora za kukabiliana na magonjwa ya mimea.

Mafunzo hayo ambayo yako chini ya Mradi wa Afya ya Mimea, yana lengo la kusaidia kufuatilia, kutabiri na kupendekeza njia bora za kukabiliana na magonjwa yanayosumbua mimea.

Dk. Michael Mahenge kutoka SUA, alisema mradi huo unafanywa kwa kushirikiana na mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali ambayo ni Shirika linalokabiliana na Viumbe Viharibifu (TPHPA) na Shirika linalojishughulisha na Kuweka Daraja la Teknolojia (RECODA).

Akizungumza Jumatano wiki hii, Dk Mahenge alisema lengo ni kuwafikia wakulima kwa urahisi hasa wale wadogo na kutekeleza kilimo chenye tija kwa kutumia mfumo wa jitihada shirikishi za kuleta mageuzi ya kilimo vijijini.

Dk. Mahenge alisema lengo la mradi huo pia ni kutatua changamoto za magonjwa ya mimea kwa kutumia teknolojia mbalimbali zikiwamo za akili bandia.

"Upatikanaji wa taarifa ni picha za majani ya mimea ili kuweza kuzitafsiri kupitia akili bandia kupata taarifa sahihi zitakazomsaidia mkulima hasa katika kukabiliana na mazao hayo.

"Atatumia teknolojia ya ndege zisizotumia rubani (Drones), simu janja na kamera za kidijitali katika mashamba ya kuanzia hekari tatu mpaka 100," alisema.

Dk. Mahenge aliishukuru serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kuendelea kufadhili miradi katika sekta mbalimbali ikiwamo ya kilimo.

Alisema teknolojia hiyo itamsaidia mkulima kufuatilia afya ya mmea tangu wakati wa kupanda mpaka kuvuna na kumwezesha kukusanya taarifa shambani kwa siku au wiki.

Vilevile mfumo huo unalenga kuwaleta wadau wa kilimo pamoja ili kuhakikisha kilimo kinachofanywa kinaleta tija kwa wakulima wadogo wa kati na wa juu.

Alisema mfumo huo unalenga kwenye mazao ya kimkakati yanayotumika kwa kilimo kama vile maharage, mpunga, mahindi na muhogo ambapo kwa Wilaya ya Mkuranga wanaangalia taarifa za zao la muhogo na mahindi.

Alisema COSTECH kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MTUSATE) umefadhili jumla ya miradi saba inayotumia akili bandia ili kutatua changamoto katika afya, kilimo, elimu na masuala ya manunuzi.

Meneja wa MTUSATE, Dk. Beatrice Lyimo, alisema mradi huo ambao unatatua changamoto ya afya ya mmea ni moja kati ya miradi iliyofadhiliwa na COSTECH kwa kushirikiana na shirika la Maendeleo na Utafiti Canada.

Alisema jumla ya Sh. milioni 150 zimetolewa kwa ajili ya mradi huo kwa matarajio ya kupata taarifa za changamoto za magonjwa ya mimea katika mazao manne yalichaguliwa zitapatikana kwa urahisi.

# Kijaji ahimiza vijana uadilifu katika ajira

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka vijana kuwa na uadilifu na kujituma wanapopata ajira viwandani ili waendelee kunufaika kwa pamoja na kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa jumla.

Dk. Kijaji alisema hayo jana alipotembelea Kiwanda cha Chemi Cotex kilichoko Mbezi Jogoo, Dar es Salaam katika eneo lenye ekari 17 na viwanda mbalimbali kuona bidhaa zinazozalishwa pamoja na kusikiliza na kutatua changamoto zinazokabili kiwanda.

"Nampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji pamoja na wafanyabiashara waliokuja kuwekeza katika viwanda na wazalisha bidhaa kwa amani na utulivu," alisema.

Dk. Kijaji alisema Dira ya Taifa ya Maendeleo itakayohitimishwa mwaka 2025 na Dira inayoandaliwa sasa, inatoa mwanga mkubwa kwa wenye viwanda kuendelea kuwekeza Tanzania kwa kuwa viwanda ni sehemu inayoajiri Watanzania wengi.

Naye Mwenyekiti wa Chemi Cotex, Yogesh Manek, alisema katika kiwanda hicho, wanazalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo dawa za meno za Whitedent na vipodozi.

"Asilimia kubwa ya Watanzania wanatumia bidhaa za kiwanda hiki na tumeajiri watu 1,000 kati ya hao, 550 wanawake na 450 wanaume huku wenye ulemavu wakiwa sita. Hii ni fursa kwa mtu yeyote anayetaka kufanya kazi," alisema Manek.

Pia alisema hali ya biashara kwa sasa ni nzuri kwa sababu wana fursa ya kufanya kazi na wanapeleka bidhaa zao Rwanda, Uganda, Kenya, Burundi,



Abiria wa mabasi yaendayo haraka wakiwa kwenye foleni ya kusubiri mabasi hayo, katika kituo cha Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana. Wakati mwingine huchelewa kufika kutokana na msongamano wa daladala kituoni hapo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mradi wa maji bil. 3.9/- kukamilika Januari

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

SERIKALI imeahidi kukamilisha mradi wa maji utakaohudumia vijiji sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 3.9.

Mradi huo unakamilishwa baada ya kudumu kwa zaidi ya miaka 15 bila kukamilika.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maji wilayani hapa ukiwamo mradi wa Chipingo ulioko kijiji cha Chipingo wilayani Masasi.

Alisema anawapongeza wananchi wa vijiji hivyo ambavyo vitafikiwa na mradi huo kwa kuwa wavumilivu kwa kipindi cha miaka mingi waliyokaa bila kupata huduma ya maji huku mradi ukiwapo bila kukamilika.

Naibu Waziri alisema serikali kwa sasa iko katika mkakati wa kukamilisha miradi yote ambayo imekaa muda mrefu bila kukamilika ili kuwezesha wananchi kupata huduma ya maji kama inavyokusudiwa.

Alisema serikali imeweka dhamira ya dhati kuhakikisha mradi huo wa Chipingo unakamilika kwa asilimia 100 na vijiji vyote ambavyo vimelengwa kupata huduma ya maji, vinaanza kunufaika mara moja.

"Sisi kama serikali tunaahidi mpaka kufikia Januari 20, 2024 mradi huu utakuwa tayari umeshaanza kutoa huduma na wananchi wataondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya maji, hivyo wananchi waondoe hofu juu ya mradi huu," alisema.

Mahundi alisema Chipingo ni moja ya miradi 167 nchini ambayo kwa miaka mingi haikukamilika ambayo kwa sasa serikali imeamua kuichukua na kuhakikisha inakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema serikali imefanikiwa kupunguza miradi hiyo iliyokwama kukamilika kutoka 167 hadi 150 ambayo tayari imeshakamilika.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Masasi, Juma Yahya, alisema katika mradi wa maji Chipingo, serikali imeshatoa mamilioni ya fedha kwa ajlli ya kukamilisha na hatimaye kuanzak utoa huduma mapema mwakani.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Saidi Kuwala, ambaye pia ni mwenyekiti wa Kijiji, alishukuru serikali kwa uamuzi wa kukamalisha mradi huo kwak uwa wananchi walikuwa wanapata adha kubwa ya upatikanaji wa huduma ya maji.

Alisema wananchi walilazimka kwenda Mto Ruvuma kuchota maji jambo ambalo limewaathiri kwa kujeruhiwa na mamba.

Mwanaidi Issa, mkazi wa kijiji hicho, alisema kukamilika kwa mradi huo kutaondoa adha kubwa ya maji ndani ya vijiji sita kikiwamo Chipingo, hivyo kuwafanya waishi maisha ya furaha kwa kupata huduma ya maji safi

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**EMMANUEL WILBUR MAYAGE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 478 DEG – NISSAN FUGA yenye jina la umiliki wa kampuni ya TRUST FARM LIMITED. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DAR/KIN/58353/2023.**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**BERNARD PETER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0960/0321 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BENJAMINI WILLIAM MKAPA HIGH SCHOOL mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/58605/2023.**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**ESTHER GODFREY MBARUKU**

anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 350 DES – TVS STAR. Chassis namba MD625AF49M1N03738. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DAR/KIN/57496/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...30/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: DAUD MATHAYO MLINGWA wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA JOHN BUGUMIYE DAUD**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 18 mwezi 12 mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO
MOROGORO

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SIMON MAXMILLIAN IRANQHE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 324 DJD – TOYOTA NOAH. Chassis namba AZR600223199. Engine namba A1Z4618200. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/ARU/ARU/5876/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 16 YA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**DANIEL SALEHE...............MAREHEMU**
**ZEFRIN DANIEL SALEHE...........MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 27 Mwezi DISEMBA, Mwaka 2023.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 21 Mwezi NOVEMBA, Mwaka 2023.

.......................................

HAKIMU MKAZI

MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

Resident Magistrate
Mwanga

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga kutinga robo fainali Afrika inawezekana

**SIMBA** na Yanga, zote kutoka Dar es Salaam ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Vigogo hao wa soka nchini wako katika hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hii ikiwa ni mara ya kwanza kwa Simba na Yanga kucheza hatua hiyo kwa pamoja.

Katika misimu minne mfululizo iliyopita, Wekundu wa Msimbazi wamefanikiwa kucheza hatua ya robo fainali wakati Yanga baada ya miaka 25 kupita, ndio wametinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Hata hivyo, Yanga ambao ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wametinga hatua hiyo baada ya miaka 25 kupita, wanacheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakiwa na 'joto' la kucheza fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita, wakishuhudia taji liliénda kwa USM Alger ya Algeria.

Tayari kila timu, zimeshacheza mechi nne za hatua hiyo ya makundi, Simba iliyopo Kundi B ina jumla ya pointi tano na iko kwenye nafasi ya pili katika msimamo wa kundi hilo wakati Yanga ambayo pia ina pointi tano iko katika nafasi ya pili, lakini imecheza mechi moja zaidi ya Al Ahly ya Misri na CR Belouizdad ya Algeria.

Simba ilifikisha pointi tano baada ya Jumanne iliyopita kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wydad Casablanca kutoka Morocco wakati Yanga iliwashindilia Medeama SC ya Ghana mabao 3-0, michezo yote ikichezwa hapa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwa matokeo hayo ya makundi yote mawili, bado nafasi ya Simba na Yanga kusonga mbele katika michuano hiyo ipo na kinachotakiwa ni wachezaji kuongeza juhudi na kujituma zaidi.

Simba na Yanga zinahitaji kupata ushindi katika michezo yao miwili iliyobakia ili kusonga mbele bila ya kusubiria matokeo yatakayohusisha wapinzani wao, ndio inawezekana kwa sababu wakishinda watakuwa wamejiongezea pointi.

Tunawakumbusha Simba na Yanga kupambana katika mechi hizo zinazofuata na ili kufikia malengo, viongozi wanatakiwa kutumia vyema dirisha dogo la usajili ambalo limefunguliwa kusajili wachezaji wenye viwango na uzoefu watakaoongeza nguvu.

Tunaamini kwa sasa tayari Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, atakuwa ameshakamilisha mapendekezo yake ya nafasi anazohitaji kuziongezea nguvu lakini anaweza kufika mbali kuwataja nyota ambao anawataka kumsaidia kufikia malengo.


Vile vile Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, ambaye ametua hivi karibuni, kupitia video za mechi zilizopita ambazo timu yake imecheza ameziangalia vyema, atakuwa ameshapata mwanga wapi anahitaji kuongeza nguvu ili itakapofika Februari, mwakani awe na kikosi imara kitakachopambana kusaka pointi sita za kuwapeleka hatua ya robo fainali.

Ni ukweli mashabiki wa soka Tanzania wanahitaji kuona timu zao au timu yao moja inatinga hatua ya nusu fainali, fainali au inatwaa ubingwa wa Afrika, mashabiki wamechoka kuwa watazamaji na mashuhuda wa kuona makombe na medali za ubingwa zikienda katika mataifa mengine. Lakini wachezaji wanatakiwa wafahamu kufanya kwao vizuri katika hatua hiyo kutaiongezea Tanzania pointi na kuipa uhakika wa kuwa na nafasi ya timu nne (mbili katika Ligi ya Mabingwa Afrika na mbili kwenye Kombe la Shirikisho Afrika), katika mashindano ya CAF msimu ujao.

Huu ni wakati wa wachezaji na viongozi kujitathmini na kuweka mikakati imara kwa ajili ya kuhakikisha ndoto na malengo ya serikali, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na wadau wa michezo yanatimia kwa kutwaa ubingwa wa Afrika.

Ili furaha hii inayoshubiriwa kwa hamu na Watanzania itimie, kila mmoja kwa nafasi yake anatakiwa kutimiza majukumu aliyopewa na kuaminiwa. Kila la heri Simba na Yanga katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayoendelea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Simba, Yanga usajili mzuri utawabeba michuano CAF

**NILICHOFIKIRIA** na kushauri wiki iliyopita kabla ya mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Simba dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco iliyochezwa Jumanne iliyopita na Yanga dhidi ya Medeama kutoka Ghana, zote zikifanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kimefanyiwa kazi.

Na matokeo ni yale yale kama nilivyoshauri kuwa iwapo timu za Tanzania zitatumia mwanya au faida iliyopo, basi zote zitapata ushindi.

Jumapili iliyopita kwenye 'Muungwana Lazima Tulonge' yenye kichwa cha habari, 'Simba itumie hali ya hewa, Yanga mashabiki kushinda mechi zao CAF', na kweli ikawa hivyo.

Na kweli ikawa kama nilivyosema, wachezaji wakapambana na Simba ikashinda mabao 2-0 dhidi ya Waarabu hao wa Morocco.

Kilichotokea ni kile kile, Yanga ilipambana na kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Medeama.

Nitoe kongole kwa wachezaji wa Simba kwa kupokea ushauri huo, kwani ni kweli walifanya vile vile.

Dakika 25 za mwanzo, Wydad Casablanca walianza kwa nguvu ili kupata mabao ambayo yangewaweka salama watakapochoka, lakini mabeki wa Simba wakiongozwa na kipa, Ayoub Lakred, walifanya kazi ya ziada kwa kutoruhusu bao, hadi dakika ya 30 walipoanza kutepeta, ndipo walipofunga mabao ya haraka haraka, na hata kipindi cha pili jua na joto vilipoungua na kufanya mashambulizi makali walikuwa wameshachelewa.

Mashabiki wa Yanga nao walifanya kazi yao nzuri iliyowapeleka kwa kushangilia kiasi cha wachezaji wa Medeama kuonekana kama hawajui wanachokifanya uwanjani.

Matokeo hayo kwa kiasi kikubwa yanazifanya timu za Tanzania kujiweka hai matumaini ya kusonga mbele hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ukiangalia kwa Simba yenyewe bila kupiga hesabu za vidole inahitaji pointi tu ili itinge hatua hiyo.

Iwapo itatoka sare ya aina yoyote dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast mechi itakayochezwa Februari 23, mwakani na Machi Mosi, mwakani ikaifunga Jwaneng Galaxy ya Botswana, moja kwa moja itakuwa inakwenda robo fainali kwa sababu itafikisha pointi tisa, na hata kama Wydad Casablanca ikishinda mechi zake mbili ilizosaliwa na kuwa na pointi tisa pia haitoweza kufuzu kwa sababu za kikanuni.

CAF wanaangalia timu zilipokutana zenyewe kwa zenyewe matokeo yake yalikuwaje kama zitakuwa zimefungana.

Kwa sababu Simba ilishinda mabao mengi dhidi ya Wamorocco hao, licha ya kufungwa bao 1-0 ugenini, kanuni itakuwa imewabeba kwani jumla ni mabao 2-1.

Kumbuka kwenye kundi hili, Asec Mimosas tayari imeshapita kwa kufikisha pointi 10

Kwa upande wa Yanga mpaka sasa ipo nafasi ya pili nyuma ya Al Ahly ya Misri, zote zikiwa na pointi tano, na zilizobaki mbili CR Belouizdad ya Algeria na Medeama zina pointi nne, hivyo katika Kundi hilo D, timu zote bado zina nafasi sawa.

Ni kiasi cha Yanga kufanya vyema kwenye mechi zake mbili, hasa ile ya Februari 23, mwakani itakayocheza dhidi ya CR Belouizdad, kabla ya kwenda kumalizia mechi ya mwisho, Machi, Mosi dhidi ya Al Ahly.

Kwa jinsi zilivyocheza na zilivyo kwa sasa Simba na Yanga zina uwezo huo, lakini kwa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili lililofunguliwa Desemba 16, zinatakiwa kufanya usajili mdogo lakini wenye tija, kuingiza wachezaji watakaoongeza nguvu kwenye vikosi.

Simba iwapo itaongeza wachezaji sehemu ambazo zina mapungufu, inaweza kabisa kwenda kushinda Ivory Coast dhidi ya Asec Mimosas, ikashinda pia mechi zake zote mbili na kupata pointi sita, achilia mbali nne zinazotakiwa.

Yanga nayo kama itaongeza nguvu pale mbele ya kusaka straika wa maana, sina shaka kuwa itakwenda kufavya vizuri kwenye mechi zake mbili zilizobaki.

Kifupi tu wawakilishi wote wa Tanzania bado wana nafasi, kinachotakiwa kujiimarisha kwa kufanya usajili ili mechi zinazokuja zicheze zikiwa na nguvu mpya.

# Katambi ataka Wajasiriamali kuchangamkia mikopo halmashauri

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amewataka wajasiriamali kuchangamkia fursa ya mikopo asilimia 10 ya halmashauri ili kujikwamua kiuchumi.

Mikopo hiyo hutokana na mapato ya ndani na asilimia nne hutolewa kwa vijana na wanawake, huku asilimia mbili ikitolewa kwa watu wenye ulemavu.

Awali, mikopo hiyo ilisitishwa na serikali kwa ajili ya kufanyiwa maboresho lakini itaanza tena rasmi mwakani.

Naibu Waziri Katambi, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na baadhi ya wajasiriamali wa Manispaa ya Shinyanga na kusema mikopo hiyo isiyo na riba itaanza kutolewa mwakani, hivyo waichangamkie ili wapate mitaji na kujikwamua kiuchumi.

"Serikali tayari imemaliza kuifanyia maboresho na Januari, mwakani, itaanza kutolewa tena. Itumieni kujikwamua kiuchumi kwa kufanya biashara mbalimbali kwa tija,"alisema Katambi.

Pia aliwakumbusha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchaguzi ujao kwa kuwachagua viongozi makini, wachapakazi na wenye kupenda maendeleo, na si kuuza maendeleo kwa kuchagua kiongozi asiyestahili kwa sababu ya rushwa.

"Kura yako ndiyo maendeleo yako, tuache kuuza maendeleo kwa pesa, chagueni viongozi wenye uchungu na nyie," alisema Katambi.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, aliwasihi wanawake wasibweteke bali waichangamkie mikopo hiyo ambayo kwa sasa itaanza kutolewa hata kwa mtu mmoja mmoja na si lazima kikundi kama zamani na waitumie kufanya shughuli za ujasiriamali.

Baadhi ya wajasiriamali walimshukuru kwa kupatiwa elimu ya ujasiriamali na fursa zilizopo, ambazo wanaweza kuzitumia na kujikwamua kiuchumi.

Kuhusu mikopo hiyo, walitoa wito kwa serikali kuondoa milolongo mirefu kuipata ili kutosababisha wanawake kuendelea kujiingiza kwenye mikopo kausha damu.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji, akikabidhi cheti cha udhamini kwa Mkuu wa Biashara wa SBC Tanzania Limited Foti Gwebe -Nyirenda, wakati wa tuzo za Rais kwa wazalishaji bora nchini (PMAYA), zilizoandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), zilizofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wafanyakazi Urafiki kicheko Serikali ikitoa mafao bil. 2.4/-

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri Tanzania (TUICO), kimesema serikali imewapatia Sh. bilioni 2.4 kwa ajili ya kuwalipa wanachama wao ambao walikuwa wafanyakazi wa kiwanda cha Tanzania China-Friendships Textile Co.Ltd (Urafiki).

Baada ya kutolewa kwa fedha hizo, uongozi wa TUICO umeanza rasmi kuhakiki majina ya wanachama kwa lengo la kuanza kuwaingizia fedha zao katika akaunti walizokuwa wakidai kuanzia mwaka 2008 hadi 2013.

Katibu Mkuu wa TUICO, Boniphace Nkatatisi, alisema juzi jijini Dar es Salaam kuwa chama kimekuwa na mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yake.

Nkatatisi alisema TUICO inaishukuru serikali kwa kutoa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya shughuli zao za chama na kuwasaidia kufanikiwa kuwalipa wafanyakazi hao.

"Tunayofuraha kubwa sana kwa chama kufanikisha kumaliza mgogoro wa muda mrefu baina ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Urafiki dhidi ya mwajiri wao na serikali," alisema Nkatatisi.

Alisema serikali imetekeleza kwa vitendo kulipa madeni ya madai ya wafanyakazi nchini na kuheshimu vyema maamuzi ya Mahakama pale ambapo wafanyakazi wameshinda mashauri yao dhidi ya serikali.

Mwanasheria Mkuu wa TUICO, Noel Nchimbi, alisema katika kipindi cha Januari mpaka Septemba, 2023, chama kimefanikiwa kushughulikia migogoro ya kazi 301.

Pia alisema chama kilishughulikia migogoro ya ngazi ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), chama kilipokea migogoro 134 na kufanikiwa kuimaliza.

Mmoja wa wafanyakazi wa Urafiki, Majuto Honelo, alisema alianza kazi mwaka 1973 hadi 2012, hivyo anaishukuru TUICO kwa jitihada ya kusimamia kesi hiyo hadi kupata haki yao.

"Tunashukuru kesi tumeshinda hadi leo kuja kuhakiki majina yetu kwaajili ya kulipwa, pia tunaishukuru serikali kwa jitihada ya kuwezesha kulipwa mafao yetu ambayo yamedumu tangu mwaka 2013 tuliposhinda kesi hadi leo tunalipwa haki zetu".

# TBS yafunda wanawake kupata alama ubora

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetumia Maonyesho ya Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kutoa elimu kwa washiriki wa maonyesho hayo ili kuwajengea uelewa kuhusu namna kupata alama ya ubora ya TBS.

Maonyesho hayo yanafanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Christopher Magafu, alisema maonyesho hayo yamekuwa fursa nzuri kwa shirika kutoa elimu kwa wajasiriamali kutokana na wengi kutokuwa na elimu ya kupata alama ya ubora.

"Hivyo kwa ushiriki wetu, tunaamini elimu hii itawarahisisha mawazo yao madogo kuwa makubwa," alisema Magafu.

Alisema serikali imewarahisishia wajasiriamali kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure, ambapo kila mwaka inatenga fungu maalum kwa ajili kuwasaidi wajasiriamali wadogo na wa kati ili waweze kutimiza ndoto yao ya kuweza kupata alama ya ubora.

Kinachotakiwa, alisema ni wao kupata vibali vinavyotolewa na SIDO na baada ya hapo, SIDO itawapa barua ya utambulisho ambayo wakiipeleka TBS basi watatambuliwa kuwa wamekidhibi vigezo vya kuitwa wajasiriamali.

"Kupitia utambulisho huo wa SIDO, mjasiriamali anaweza kufanya maombi kupitia mfumo unaopatikana kwenye tovuti ya shirika letu, wakiingia wataona sehemu ya kuingia na kutuma maombi yao bila sumbufu wowote," alisema.

Awali, akifungua maonyesho hao, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, aliwataka wanawake kutoacha kuchangamkia fursa za mikopo isiyo na riba ambayo inatarajiwa kuanza kutolewa hivi karibuni.

Zungu alisema mikopo hiyo, awali ilisitishwa na inatarajiwa kurudi tena hivi karibuni kwa utaratibu maalumu, huku akiwasisitiza wanawake hao kutoiacha fursa hiyo.

"Mikopo ambayo iliondolewa itarudi hivi karibuni kwa utaratibu maalumu, hivyo napenda kuwasisitizia wanawake msiache kuitumia fursa hii, kwani mikopo yake haina ukomo wa umri kwa wanawake", alisema Zungu.

Pia alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Jomaary Satura, kupinga vitendo vya uonevu vinavyofanywa na baadhi ya watu dhidi ya wajasiriamali, hususani wanawake katika maeneo ya kufanyia biashara.

# UNFPA yakumbuka waathirika mafuriko

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, limetoa msaada wa vitu vya usafi kwa wanawake na wasichana manusura wa mafuriko ya mvua wilayani Hanang mkoani Manyara.

Baadhi ya vitu hivyo ni nguo za ndani, pedi, sabuni ya kuogea, sabuni ya kufulia, dawa ya meno na mswaki, huku Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Mark Bryan Schreiner, akisema, wanawake na wasichana ni miongoni mwa watu 5,600 walionusurika katika mafuriko hayo.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana baada ya kutoka Hanang kutoa msaada huo, Schreiner alisema msaada walioutoa ni muhimu kwa makundi hayo.

"UNFPA ilikabidhi msaada wa vitu hivyo ambao umepokelewa Kanali Selestine Masalamado ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Operesheni na Uratibu katika Idara ya Udhibiti wa Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya serikali," alisema.

Schreiner alisema, mbali na usalama na ulinzi, wanawake na wasichana walioathiriwa na mafuriko hayo ni muhimu wapate huduma bora za afya, na kwamba ndio maana wamepeleka msaada wa vitu hivyo.

"Wakati Tanzania inakabiliana na athari za mvua zilizo juu ya wastani katika maeneo mbalimbali, UNFPA inaahidi kuendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine kutoa msaada wa kiutu," alisema.

Aidha, alisema UNFPA Tanzania inajishughulisha na huduma za kiutu, afya ya uzazi, vita dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo mbalimbali ikiwamo kambi ya wakimbizi Kigoma

"Lakini pia UNFPA inafanya kazi ya huduma za kibinadamu katika nchi zaidi ya nchi 60 ulimwenguni na imekuwa ikishirikiana kwa karibu ba serikali za nchi husika," alisema.

# Sheria majengo mwarobaini gharama ujenzi

**Na Mwandishi Wetu**

KUKOSEKANA kwa sheria moja inayosimamia shughuli za ujenzi wa majengo, kumeelezwa kuwa chanzo cha kusababisha gharama kubwa za ujenzi nchini.

Ili kuondoa tatizo hilo, imeshauriwa kuwapo kwa sheria moja ya ujenzi ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kupunguza gharama za ujenzi zinazolalamikiwa na wananchi kwa muda mrefu.

Mhandisi Ujenzi wa Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), Geofrey Mwakasenga, amesema katika kukabiliana na hali hiyo, tayari baraza hilo limekamilisha mchakato wa kuandaa andiko linaloainisha umuhimu wa sekta ya ujenzi, hivyo kuwezesha kutungwa kwa sheria itakayosimamia shughuli zote za ujenzi wa majengo nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Kkitendo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Ujenzi, hatua hiyo inatokana na uamuzi wa serikali kupitia wizara hiyo kuandaa mfumo bora wa kisheria, kanuni na miongozo.

Taarifa hiyo ilisema vitu hivyo vitasimamia ujenzi wa majengo nchini, hivyo kuwezesha sekta ya ujenzi kuwa na sheria moja inayoongoza shughuli zote za majenzi hatimaye kuondokana na utaratibu wa kuwa na sheria nyingi zinazosimamia sekta na kuongeza gharama za ujenzi.

"Uwapo wa sheria ya majengo nchini utawezesha kuwapo kwa mfumo wa pamoja wa usimamizi wa ujenzi wa majengo wenye uwezo wa kudhibiti uharibifu wa mazingira, ubora, usalama na afya katika sekta ya ujenzi," alisema Mhandisi Mwakasenga.

Amezitaja sheria zinazosimamia ujenzi wa majengo nchini kuwa ni sheria za mipango miji, sheria ya afya na usalama mahali pa kazi, sheria ya zimamoto na uokoaji, sheria ya mazingira, sheria ya ukandarasi na usajili pamoja na sheria zinazosimamia taaluma na wataalamu katika fani za uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

Changamoto zinazoikabili sekta ya majenzi kwa sasa ni kutosimamiwa vizuri kwa miongozo ya ujenzi, ubomoaji wa majengo kutosimamiwa ipasavyo na kutokua na viwango vya kitaifa vya majengo nchini.

Mhandisi Mwakasenga alisema NCC inaendelea kutoa ushauri na msaada wa kitaalamu kwa wadau wa sekta ya ujenzi nchini kuhusu mambo yanayohusiana na sekta hiyo pamoja na kuhamasisha na kuweka mikakati ya kukuza, kuendeleza na kupanua sekta husussani kwa kujenga uwezo na ushindani wa wazawa ili waweze kushindana na kutekeleza miradi kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), ni chombo kinachohusika na uratibu wa sekta ya ujenzi nchini pamoja na uchagizaji wa maendeleo ya sekta hiyo kwa ujumla na lilianzishwa mwaka 1979 kwa Sheria ya Bunge Na. 20 na lilianza kutekeleza majukumu yake rasmi mwaka 1981.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mwamini Juma, akiwaonyesha wajumbe wa bodi hiyo sukari ya awali iliyoanza kuzalishwa na kiwanda cha Mkulazi kinachomilikiwa na mfuko huo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Kiwanda cha sukari Mkulazi chaanza uzalishaji wa awali

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

KIWANDA cha Sukari cha Mkulazi kilichoko Kilosa mkoani Morogoro kimeanza uzalishaji wa awali wa sukari huku Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambao ndio wamiliki ikiwahakikishia wanachama wake usalama wa fedha zao na kutaja kuwa zitarejea kwa wakati.

Kiwanda cha sukari cha Mkulazi kinamilikiwa na NSSF yenye asilimia 96 na Jeshi la Magereza asilimia nne kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea kiwanda hicho, Mwenyekiti wa Bodi ya NSSF Mwamini Juma, alisema uzalishaji huo wa awali utasaidia kupunguza uagizwaji wa sukari kutoka nje ya nchi.

Alisema kuwa kiwanda hicho licha ya kutoa zaidi ya ajira 5,000 pia kitazalisha sukari ya viwandani (brown sugar) ambayo hakuna kiwanda kingine chochote nchini kinachoweza kuzalisha pamoja na kuzalisha sukari ya kawaida.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Mkulazi, Dk Heldelitha Msita, alisema bodi ya NSSF imetembelea kiwanda hicho na kuridhika na hatua iliyofikiwa ya kukamilika kwake na kwa sasa kipo katika hatua za majaribio ya mwisho kwenye uzalishaji.

"Bodi ya NSSF ilitupa kazi ya kusimamia ujenzi wa kiwanda hiki cha Mkulazi. Leo (jana) imetutembelea na kuona kazi waliyotupa tunaendelea kuimaliza. Kwa sasa tuko kwenye majaribio ya mwisho katika uzalishaji na muda wowote kuanzia sasa bidhaa ya sukari itaanza kuonekana mitaani," alisema Dk. Msita.

Naye Mtendaji Mkuu wa Kiwanda, Selestine Some, alisema kiwanda hicho ni cha kipekee kitazalisha sukari ya kipekee ya viwandani ambayo haizalishwi na viwanda vilivyopo kwa sasa nchini.

Alisema tangu ujenzi wa kiwanda hicho uanze na mpaka utakapokamilika zaidi ya ajira 5,000 zitatolewa katika ngazi mbalimbali zikiwamo za muda na zile za kudumu.

Some alisema mpango mkakati wao ni kulima na kupanda miwa eneo lenye ukubwa wa hekta 4000 na kukamilisha mifumo ya umwagiliaji na kununua vifaa na zana za kilimo za kisasa.

Mtendaji Mkuu huyo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassani kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya uwekezaji wake kwa kuwa utasaidia kupunguza uagizwaji wa sukari kutoka nje.



HABARI DODOMA

# Machali aagiza ufaulu uongezeke

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali amewaagiza maofisa elimu wa wilaya, kata na walimu kujitathimini utendaji kazi wao na kuelekeza nguvu kuinua kiwango cha taaluma na ufaulu wilayani hapa.

Machali alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na maofisa elimu hao na walimu katika kikao cha kutathimini hali ya ufaulu wa mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi uliofanyika nchini mwaka huu.

Alisema iwapo kila mmoja atatekeleza majukumu yake vizuri watachochea ongezeko la ufaulu kwa wanafunzi na hivyo kujiweka katika nafasi nzuri ya kimkoa na taifa.

"Nendeni mkasimamie majukumu yenu kikamilifu, ofisa elimu, mratibu elimu kata na mwalimu kila mmoja akiwajibika vizuri katika nafasi yake kiwango cha elimu katika wilaya yetu kitapanda ukilinganisha na sasa na kujiweka mahali pazuri kimkoa," alisema.

Vilevile, aliwagiza walimu wilayani hapa kutumia ardhi ya shule katika kipindi hiki cha mvua za masika kulima mazao na kupata chakula cha kuwapa wanafunzi kila siku.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, alisema wameweka mikakati ya kuimarisha na kuboresha usimamizi wa mifumo ya ufuatiliaji pamoja na kutoa motisha kwa wanafunzi na walimu wanaofanya vizuri katika taaluma.

Asia, alisema katika mkakati huo wanafunzi wanaofanya vibaya katika mitihani, watatambuliwa kwa kuwapa zawadi hadi itakayowafanya wajitathimini na kuongeza juhudi katika masomo yao.

Aliwagiza watendaji kata, waratibu elimu kata na kamati za shule kuwachukulia hatua za kisheria wazazi wanaoshindwa kusimamia mahudhurio ya watoto wao shuleni Ili kudhibiti utoro kwa kuwa unazorotesha elimu.

Awali Kaimu Afisa Elimu Shule ya Msingi wa Halmashauri hiyo, Amina Irumba, alisema halmashauri imeongeza ufaulu kwa asilimia 2.7 kwa kupata asilimia 68.30 mwaka huu ikilinganishwa na wa mwaka 2022 asilimia 65.52.

Alisema ufaulu kimasomo unaonyesha watahiniwa wamefaulu kwa kiwango cha juu kwa somo la Kiswahili kwa asilimia 77 huku Kiingereza na Hisabati ikiwa chini ya asilimia 50.

# Silaa: Tunalalamikiwa sana ugawaji ardhi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa ameitaka menejimenti na taasisi zilizopo chini ya wizara yake kufanya kazi kwa kujua mwonekano wao ulivyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan na kuondoa malalamiko mengi dhidi yao katika ugawaji, umilikishaji na upokaji ardhi wananchi.

"Tunapofanya kazi tujue kwenye maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, sisi sura yetu kwa kiongozi mkuu wa nchi ikoje, tunalalamikiwa sana, watu wengi wanadhulumiwa ardhi zao kupitia mikono yenu, kujimilikisha ardhi kinyume cha utaratibu, kugawa maeneo zaidi ya mara moja, mkabadili hali hii watu wazungumze tofauti," alisema.

Akizungumza wakati wa mkutano wake na menejimenti na taasisi hizo ikiwa ni tathimini ya siku 100 tangu ateuliwe kushika wadhifa huo, alisema amezunguka mikoa 23 na vijiji 975 na kuelekeza maofisa ardhi wanapotaka kumiliki ardhi wapewe mamlaka ya kumilikishwa na ofisa mwingine.

"Agosti 30, 2023 Rais Samia Suluhu Hassan alinipa dhamana na Septemba Mosi aliniapisha na kutoa maelekezo mahususi na alipenda kuona nakwenda kusimamia mageuzi kwenye wizara ili kufikia malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kuna maelekezo anayotoa mara kwa mara," alisema.

Silaa aliwataka maofisa hao kwenda kufanya kazi na kuleta sura mpya ya wizara kutokana na malamiko mengi ikiwemo maofisa ardhi kujimilikisha maeneo ya wananchi.

"Mkafanye kazi ili Rais siku moja aseme mashauri ya ardhi yamepungua, tuepuke lile la kila mtu anayetaka huduma lazima aanzie kwa waziri," alisema.

Alisema baada ya kuapishwa bungeni alihidi kupita vijiji 975 na mikoa ndani ya siku 100 kusimamia utekelezaji wa maagizo na kukutana na watendaji wanaofanya kazi na timu za ardhi kwenye mikoa, wilaya na halmashauri ili kuhakikisha timu ya wizara inatekeleza maagizo ya Rais Samia.

"Nimefanikiwa kwenda kwenye mikoa 25, sijafika Ruvuma peke yake, Njombe nimepita mara mbili, Manyara nilifika wakati wa tukio la Katesh, lakini

mikoa 23 nimefika na kukagua ipo mikoa nimekwenda mara mbili," alisema na kuongeza:

"Nimekwenda Sumbawanga mara mbili, Arusha zaidi ya mara mbili, Katavi, Lindi na Mtwara pia,

Alisema siku 100 ni chache na kuna vikao vya Bunge ambavyo anatakiwa kuhudhuria, lakini alifanya kazi na katika mizunguko hiyo, amejifunza na kutoa maagizo.

Kwa mujibu wa Silaa, Septemba 4, mwaka huu, alikutana na menejimenti ya wizara hiyo na kutoa maelekezo yenye vipengele 12.

Aliwakumbusha wataalamu wa ardhi waliopo mikoani kuhakikisha maagizo yake yanafanyiwa kazi ili kuondoa malalamiko kwa wananchi.

Alisema miongoni mwa maagizo hayo ni kutaka siku 100 zitumike kwa kufanya mabadiliko, kutatua migogoro, kuzungumza na wateja na kurejesha imani kwa wizara.

"Principle (kanuni) zangu zinaamini kila mtu ni mtaalamu anafanya kazi aliyoisomea, nikiondoa yale madhaifu ya kibinadamu ya bahati mbaya, naweza kuvumilia makosa ya mtu, lakini ya makusudi yanaleta chuki kwa wananchi, hawezi kubaki nayo na mtu anayemuhukumu atamuhukumu Rais Samia Suluhu Hassan," alisema

Kwa upande mwingine, alisema wamewasimamisha kazi watumishi 13 wakiweno tisa wa Halmashauri wa Jiji la Dodoma, wawili Dodoma kwa tuhuma za kukiuka sheria.

Aliwata maofisa ardhi wanapotaka kumiliki ardhi wapewe mamlaka ya kumilikishwa na ofisa mwingine kwa kuwa hakuna utaratibu wa wao kuwa jaji kwenye kesi yao wenyewe.



Takataka zikiwa zimerundikwa kwenye dampo lililopo pembezoni mwa wafanyabiashara wa stendi ya daladala ya Sabasaba Jijini Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaongeza usalama mifumo ya taarifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Benedict Ndomba amesema wamefanikisha ujenzi wa mifumo ya serikali ya kuwasiliana na kubadilishana taarifa wa GovESB ili kuongeza usalama wa taarifa.

"Mfumo huu umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kuzingatia kifungu cha 48 (2) cha sheria ya serikali mtandao namba 10 ya mwaka 2019 kinachoitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao kuanzisha na kuendesha mfumo unaowezesha mifumo ya TEHAMA serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa," alisema Ndomba

Alisema sambamba na kutekeleza matakwa hayo ya kisheria, ujenzi wa mfumo wa GovESB ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika taasisi za umma inaounganishwa na kubadilishana taarifa.

"Mfumo wa ubadilishanaji taarifa serikalini ni mfumo wa kielektroniki unaounganisha mifumo ya TEHAMA ya taasisi za umma iweze kusomana na kubadilishana taarifa kila inapohitajika,"alisema.

Kadhalika, alisema lengo la mfumo huo ni kuziwezesha taasisi za umma kubadilishana taarifa kidijitali kwa usalama, kupunguza udurufu wa mifumo, kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, kupunguza gharama za uendeshaji na kuokoa muda kwa taarifa kupatikana kwa wakati. Alisema kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo wa GovESB, kulikuwa na changamoto za ubadilishanaji wa taarifa za umma, ikiwemo kutumia muda mrefu kupata taarifa kwakuwa taasisi zililazimika kuwasilisha maombi ya kupata taarifa kwa njia ya barua.

"Utaratibu huu wa barua ulichukua muda mrefu kupata taarifa hizo jambo lililochangia kupunguza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi," alisema

Aliitaja changamoto nyingine kuwa ni utofauti wa kupata taarifa kutoka taasisi moja hadi nyingine kutokana na kutofautiana kwa utaratibu wa ndani wa kupata na kutoa taarifa na wakati mwingine kubadilika.

"Hapo awali ili mifumo ya TEHAMA iweze kusomana ililazimika kuunganisha mfumo mmoja kuzungumza na mingine kila inapohitajika uunganishwaji huu ulisababisha udurufu wa mifumo, kupunguza ufanisi wa mifumo na kuongeza gharama za usimamizi na uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA," alisema

Alisema kupitia GovESB changamoto hizo zimetatuliwa na sasa taasisi zote zinabadilishana taarifa kupitia mfumo huo kwa wakati na kwa usalama zaidi. Alisema mfumo huo umesaidia kuokoa muda wa kuwahudumia wananchi na kupunguza gharama za kutengeneza mifumo midogo ya TEHAMA inayounganisha na ya taasisi nyingine.

Hata hivyo, alisema hadi sasa taasisi 109 zimeunganishwa katika mfumo huo na mifumo 117 imesajiliwa.

"Miongoni mwa taasisi hizo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Leseni za Biashara (BRELLA) na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA)," alisema.





## Atoa mbinu kupunguza mzigo hospitali rufani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ili kuipunguzia mzigo hospitali ya rufani ya Mnazi Mmoja ni vyema wananchi wakafuata mfumo wa rufani unaopendekezwa na wataalamu wa afya.

Othman alisema hayo jana wakati akifungua hospitali ya wilaya Chumbuni ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Alisema hospitali hiyo ni mkombozi mkubwa kwa wananchi wa maeneo hayo na ya jirani na huduma za kibingwa zitapatikana, hivyo hakuna haja ya kufuata huduma hizo katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja.

Othman alisema lengo kuu la uwapo wa hospitali hiyo ni kuimarisha mfumo wa rufani na kuwapunguzia wananchi mzigo wa gharama za kufuata matibabu masafa marefu mbali na maeneo wanayoishi.

Alisema ili kufikia dhamira ya kutoa huduma bora na endelevu kwa wananchi, serikali kupitia Wizara ya Afya imeanza ushirikiano na sekta binafsi katika baadhi ya maeneo ya utoaji wa huduma za afya ndani ya hospitali zikiwamo za uchunguzi na uendeshaji wa hospitali.

Serikali, alisema itaendelea kufanya hivyo kwa yale maeneo ambayo watahisi utekelezaji wake utaimarika zaidi.

Pia alisema wizara imeshafanya tathmini ya mahitaji ya wafanyakazi wa fani zote wanaohitajika katika hospitali hiyo kwa mujibu wa kada zao wakiwamo madaktari, wauguzi, wataalamu wa uchunguzi na kada zingine muhimu zinazohusiana na utoaji wa huduma zilizoainishwa ili hospitali hiyo kufikia malengo.

Aliutaka uongozi wa Wizara ya Afya, watendaji na wafanyakazi wa hospitali hiyo kuhakikisha utunzaji na ukarabati wa miundombinu na vifaa kwa wakati ili kuwaepushia usumbufu wananchi na kuhakikisha huduma zinatolewa bila ya kusuasua.

Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alimpongeza Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa uamuzi wake wa kuimarisha sekta ya afya hasa katika ujenzi wa hospitali kila wilaya na kwamba kwa kiasi kikubwa zitasaidia wananchi kupata huduma katika maeneo yao.

Aliwataka wafanyakazi wa hospitali hiyo kutoa huduma bora ili wananchi kupata matibabu ya haraka na kuepusha malalamiko yasiyokuwa ya lazima.

# Zanzibar kuweka mazingira bora uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali ina mikakati ya kuimarisha uwekezaji ili kuwa na mazingira bora yanayowavutia wawekezaji.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa Hoteli ya Mada yenye hadhi ya nyota tano iliyoko Michamvi, mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hemed alisema serikali inaendelea kuimarisha na kujenga miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege sambamba na kuimarisha upatikanaji wa nishati, maji safi na salama na huduma zingine za kijamii ili kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji.

Alisema ujenzi wa hoteli hiyo inayomilikiwa na kampuni ya Mada Hotels Tanzania, hadi kukamilika kwake unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani 6,500 na itakuwa na vyumba 100 vya kulaza wageni na kusaidia kuzalisha zaidi ya ajira 200.

Makamu wa Pili wa Rais aliwataka vijana ambao watapata ajira katika hoteli hiyo kuwa waaminifu na kufanya kazi kwa bidii ili waendelee kuaminika katika majukumu watakayopangiwa.

Sambamba na hilo, aliwataka wawekezaji wa hoteli kutekeleza wajibu wao hasa katika kulipa kodi stahiki, kuwatendea haki wafanyakazi pamoja na kushirikiana na wananchi wanaoishi maeneo yanayowazunguka ili kudumisha amani na utulivu. Alisema serikali imekusudia kutoa kila aina ua ushirikiano kwa wawekezaji wote wanokuja Zanzibar na kufanya hivyo ni kuimarisha uchumi wa Zanzibar na kuongeza nafasi za ajiri kwa vijana.

"Wawekezaji wanokuja kuwekeza katika miradi mikubwa ya maendeleo lazima kuthaminiwa na kupewa kipaumbele katika kuwahudumia," alisema Hemed.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, aliwataka waliopewa maeneo kwa ajili ya uwekezaji, kuyatumia kama walivyopangiwa na serikali na kuacha tabia ya kutoyatumia hatimaye kuwa magofu jambo ambalo linarejesha nyuma malengo ya serikali. Soraga alisema sheria mpya ya uwekezaji ambayo inatarajiwa kutiwa saini hivi karibuni, imeainisha hatua zitakazochukuliwa kwa mwekezaji ambaye atazuia eneo la uwekezaji pasipo kulifanyia shuhuli stahiki ikiwa ni pamoja na kurudishwa serikalini eneo na kupewa wawekezaji wengine kwa maslahi ya taifa.

Waziri huyo alisema Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) inafanya kazi kwa haraka na ufanisi mkubwa ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma katika mamlaka hiyo unakuwa wa rahisi na kwa wakati muafaka.

Mkurugenzi Mtendajeji wa ZIPA, Sharif Ali Sharif, alisifu juhudi za mwekezaji huyo kwa kuendelea kuiamini Zanzibar na kufanya uwekezaji mkubwa ambao utatoa ajira nyingi kwa wazawa na kuipatia pato serikali. Alisema hatua hiyo itasaidia kukuza uchumi wa Zanzibar na taifa kwa ujumla.




Dereva wa Fuso akipimwa kiwango cha ulevi, eneo la Rufiji mkoani Pwani juzi, huku Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabani nchini, Ramadhan Ng'azi akishuhudia, ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na ajali wakati huu wa kuelekea mwisho wa mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi asisitiza mabadiliko kidijitali katika sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amesema mabadiliko ya kidijitali katika afya ni mojawapo ya malengo muhimu zaidi ya utawala na lazima yatimizwe kwa ushirikiano wa pande zote.

Amesema hatua hiyo ni muhimu kufanyika vizuri ili kuepuka matokeo mabaya kama makosa ya matibabu ambayo ni sababu ya saba ya vifo duniani.

Aliyasema hayo jana katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, katika uzinduzi wa jumuiya ya HODARI Initiative Organization uliofanyika visiwani hapa.

Dk. Mwinyi alisema kwa muda mrefu serikali kwa kushirikiana na wadau wa kimataifa ikekuwa ikikusanya takwimu kwa gharama kubwa na umefikia wakati kila kitengo cha afya kujiimarisha kuzitumia.

Alisema fedha nyingi zinatumika katika kupunguza vifo na magonjwa kama vile Ukimwi, kifua kikuu na malaria na kuweka kuepusha makosa yanayojitokeza wakati wa matibabu.

Alisema ni muhimu wafanyakazi wa sekta ya afya kujiongeza wakiwa sehemu zao za kazi kupitia elimu endelevu na kubadilisha mwelekeo wa matumizi ya taarifa za afya kwa njia ambayo itaboresha utendaji katika enzi hizi za kidijitali.

"Nimeona waziwazi jinsi taasisi hii itakavyokuwa njia moja ya kuongeza ufanisi kwenye taarifa na mifumo na ikiratibiwa vizuri katika kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi, tutapiga hatua madhubuti kwenye maendeleo ya afya," alisema.

Alisema Wizara ya Afya na wataalamu wa HODARI wanaweza kubuni mapendekezo ya maendeleo ya wafanyakazi ili wafanikiwe kwa kiwango cha juu zaidi bila ya watu sahihi, hata mifumo imara hukosa kupatikana faida yake.

Pia alisema mataifa ya Afrika yanaweza kuwa nyuma katika kupata uzoefu wa teknolojia katika sehemu ya huduma lakini kuongezeka kwa uvumbuzi na teknolojia kunaleta matumaini.

"Kuna utayari katika kubadilisha afya kuwa ya kidijitali kutoka ngazi ya mgonjwa binafsi hadi ngazi ya jamii. Watu wengi wanatumia muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii bila kupata mafunzo rasmi ya kufanya, hivyo na muda huo kwa siku unaweza kutumika kufuatilia afya ya mtu, kujikinga na magonjwa yanayo ambukiza na yasiyoambukizwa," alisema.

"Wakati kama huu kila mwaka, tunapima matokeo ya shughuli zilizofanywa na kurekebisha kulingana na matokeo ya utafiti. Tunatarajia kuona ushirikiano mkubwa na taasisi zetu za elimu na jamii katika kujibu maswali ya utafiti yanayobadilisha," alisema Dk Mwinyi.

Mkurugenzi wa HODARI, Zeyana Abdallah, alisema lengo la taasisi hiyo ni kuungnaisha nguvu kwenye mpango wa utafiti wa taarifa za kiafya kwa njia ya kidigitali na kutoa suluhisho kwenye afya ya jamii.

Alisema taasisi hiyo inaangalia afya ya kidigitali kama bidhaa muhimu inayoendana na maen-

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI DESEMBA 23, 2023



CHINO
UKURASA 12



# AMEFICHUA KILICHOFICHWA

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Vanessa Mdee amefichua siri ambayo wasanii wengi wa muziki hawataki kuisema wanaishi nayo kila siku na hatimaye wanaishia pabaya.

Vanessa ameweka wazi kwamba wakati akiwa katika kilele cha mafanikio katika muziki, maisha yake yalitawaliwa na ulevi wa kupindukia na msongo wa mawazo.

Amesema matumizi ya vinywaji vikali ilikuwa sehemu ya maisha yake na alijikuta akiingia huko kutokana na kukabiliana na msongo wa mawazo uliokuwa ukimkabili.

Msanii huyo mwenye kipaji cha kuimba na kucheza, amesema alikuwa akinywa pombe kupita kiasi na ilifikia hatua hawezi kulala bila kupata kinywaji chenye kilevi ili kumtuliza akili.

“Nilipokuwa kwenye tasnia ya burudani, nilikuwa na msongo wa mawazo na ili kukabiliana nao, nilikunywa pombe kupita kiasi. Nilikuwa mlevi wa kupindukia,@ amesema

Amesema  mwanzo alikuwa akifanya kazi kikamilifu, lakini mwaka wa 2018 ulikuwa mwaka wa hatari kwake kwani alikunywa kila siku ili kupata usingizi na kwamba yalikuwa maisha yasiyofaa.

“Nilikunywa kila usiku ili kwenda kulala na ilikuwa maisha yasiyofaa, “amesema kupitia mtandao wa TikTok.

Amesema kabla hali haijawa mbaya, aliamua kujitafakari kuhusu maisha yake na kuamua kumrudia Mungu ambaye amemsaidia kubadilika.

“Nilipomkaribia Mungu, Roho Mtakatifu alinitia hatiani kuacha pombe na baada ya uzoefu wa kibinafsi na  kiwewe niliamua kuacha kunywa milele.”

Vanessa ambaye kwa sasa ni mama watoto wawili anaishi Marekani na mchumba wake raia wa Nigeria, Rotimi ametangaza kuacha muziki.

BASI SAWA

## Jay Willz atamani kuichezesha Dar



MWANAMUZIKI wa Nigeria Jay Willz, anatarajia kupanda jukwaani kuwaburudisha wakazi wa Dar es Salaam katika mkesha wa Sikukuu ya Krismas.

Jay Willz anatarajiwa kutumbuiza katika kiwanja cha burudani kinachojulikana na wengi Kidimbwi Beach kwenye ufuo wa bahari ya Hindi.

Staa huyo alishirikishwa kwenye collabo na Diamond katika ngoma inayoitwa Melody ambao umepata mashabiki wengi katika mtandao wa Youtube.

## Shetta akubali yaishe kwa Qayllah



MWANAMUZIKI Mkongwe wa Bongo Fleva, Shetta amesema binti yake Qayllah anaweza kufika mbali katika siasa kwa sababu tangu mdogo hakuonyesha mapenzi katika muziki.

Amesema mtoto wake ambaye amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chipukizi CCM Taifa, alikuwa na mapenzi na siasa tangu akiwa na miaka mitatu na hapo ndipo alipogundua hawezi kufanya kazi kama yake ya muziki.

"Qayllah alipokuwa na umri wa miaka mitatu alikuwa akiimba wimbo wa CCM, nikagundua ana mapenzi ya siasa na hata alipochaguliwa nafasi hiyo nilifurahishwa kwa sababu huko ndiko anataka kwenda," amesema Shetta.



# CHINO KWA HILI UTAJENGEWA SANAMU

KAMA mradi wa ujenzi wa nyumba unaofanywa na mwanamuziki wa Bongo Fleva, Chino, utakamilika basi utamweka katika historia ya kutukuka ya kuwa mmoja wa watu waliotekeleza ahadi kwa ukamilifu.

Chino yuko mbioni kukamilisha ujenzi wa nyumba mbili ikiwa kama zawadi kwa mama yake na mama wa rafiki Nabil ambaye alifariki kwenye ajali ya gari wakati wakielekea mkoani Tanga.

Nyumba zote mbili zimejengwa eneo la Gongolamboto Kivule, kitendo hicho kinamfanya Chino kuonyesha msanii wa kipekee nchini ambaye ameweza kuenzi na kukumbuka mazuri aliyofanyiwa na rafiki yake.



## Akothee aumiza kichwa kwa baba watoto

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Esther Akoth, maarufu kama Akothee amesema malezi ya watoto yana changamoto nyingi hasa inapotokea baba anapokuwa mtata.

Mwimbaji huyo mwenye umri wa miaka 43, amesema hayo wakati akiwapokea watoto wake wawili ambao wanaishi Ufaransa na mzazi mwenzake wa mwisho, Dominic Decherf, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta.

Amesema anapata changamoto za malezi kutoka kwa mzazi mwenzake wa pili, Markus anayejulikana kama Papa Ojwang ambaye anatoka Uswizi na kusababisha kila wakati kuwa na migogoro.

FILAMU

## Nazi: Ungia mboga, wali, siyo uchawi

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU yetu ya leo tunayoiangalia inaitwa 'Nazi.' Maudhui ya filamu hii ni tabia iliyojengeka miongoni mwa jamii ambapo kuna vijana hawataki kujishughulisha na kazi yoyote kwa vile tu baba zao wana mali au nyumba.

Hawa ni hatari sana kwani huombea wazazi wao mabaya, ikiwemo wafariki dunia ili warithi.

Wazazi wao wanapobarikiwa kuwa na umri mrefu wao wananuna, na hata wengine wanataka kuwatoa roho.

Wanapofariki kwa amri ya Mungu, vijana hawa huleta matatizo kwa ndugu zao kutaka kuwadhulumu mali, au kujifanya wao ndiyo zaidi kuliko wengine.

Bayo, Warda na Erick wamezaliwa na baba mmoja, lakini Warda na Erick mama zao tofauti. Mara tu baba yao alipofariki mzozo ukaanza. Bayo kwa sababu yeye ni mkubwa na mwanaume, akataka kuwa msimamizi wa mali na nyumba ya baba yao.

Hata hivyo baba yao mdogo akawaambia kuwa alipewa usia na marehemu kuwa Warda ndiye awe msimamizi kwa sababu Bayo hakumuuguza wakati wa ugonjwa wake.

Madaraka aliyopewa Warda yalimuumiza sana Bayo na akalalamika sana, lakini hakuwa na la kufanya.

Akaona bora aende kwa mganga wa kienyeji ili kuwadhuru ndugu zake Warda na Erick.

Mganga akamwambia aende kesho yake. Halafu Mganga huyo mwenye huruma akamfuata baba mdogo wa Bayo na kumueleza tabia ya kijana wake na madhumuni yake ya kutaka kuwadhuru ndugu zake ili arithi mali peke yake.

Akamwambia baba mdogo kuwa asiwe na wasiwasi amuachie yeye kazi hiyo.

Kesho yake Bayo alipokwenda akapewa kazi akaivunje mlangoni. Akafanya hivyo. Kumbe haikuvunjika.

Erick, kijana wa miaka saba au nane, akaiokota na kumpa baba yake aungie maharage. Haikuvunjika. Mwanzoni alidanganya ya kuwa aliokota pesa akainunua. Dada yake akaenda kugombana na mwenye genge ambaye aliapa kuwa hajamuuzia dogo nazi.

Bayo akaanza kuona mauzauza na hayo yote yalitokana na nazi aliyopewa ambayo haikuwa ya kawaida, na ilikuwa ya kuwalinda Warda na Erick na si kuwaangamiza.

Hali inazidi kuwa mbaya anakimbilia kwa baba yake mdogo kwenda kuomba msamaha. Baba yake mdogo akamwambia anafahamu kila kitu juu ya yeye kwenda kwa mganga kutaka kuwaua ndugu zake.

Bayo anaahidi hatorudia tena, ndugu zake wanamsamehe, mganga anamrudisha kwenye hali yake ya kawaida, na akakubali matokeo.



# HIZI NI NGOMA ZA KRISMASI, MWAKA MPYA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA tulivyoendelea kusema na tunavyoendelea kuandika kuwa muziki wa dansi ndiyo muziki pekee ambao hauachi kitu chochote kwenye jamii bila kutungia wimbo.

Zikija sikukuu za kidini iwe Idd El Fitri au Krismasi, nyimbo zinazotamba ni za muziki wa dansi tu. Hata mwaka mpya pia, huwezi kukuta ngoma za bongo fleva zikizungumzia mambo ya mwaka mpya. Na hii kama tunavyosema kila siku ni kwamba wasanii wengi wa bongo fleva wamejikita mno kwenye nyimbo za mapenzi zaidi kuliko za matukio ya kijamii, kiserikali, maonyo na hata sikukuu za kiserikali na kidini.

Tunaelekea kwenye kipindi cha Krisimasi Jumatatu, na Jumanne. Kwa miaka mingi wanamuziki wa dansi wameendelea kuonyesha kuwa walikuwa bora zaidi, kwani una nyimbo zinazozungumzia sikukuu ya mwaka mpya.

**1. Sikukuu Imefika-George Peter**

Ni wimbo ambao hutamba sana wakati wa sikukuu za Krisimasi na mwaka mpya. Wimbo huu umetungwa na George Peter akiwa na bendi yake ya Jobiso, baada ya kutengana na kaka yake Wilson Peter Kinyonga kwa muda mfupi kabla ya kurejea tena Simba Wanyika.

Huu ndiyo wimbo maarufu zaidi wa Jobiso na baadhi ya watu hudhani ni wa Simba Wanyika.

Maudhui ya wimbo huu yanasema kuwa sikukuu ya Krismasi imefika na mwaka mpya unafika, hivyo watu wote wapite salama.

Mtunzi anamuomba Mungu awalinde wote waliobaki, kwani wakati sikukuu hizo zinafika wengine wako hospitali, wapo waliofungwa na wengine wamekufa, hivyo anamuomba Mungu waliobaki wote awasaidie uzima na afya.

**2. Tufurahi Mwaka Mpya-Hamza Kalala**

Ni wimbo ambao Hamza Kalala anawahimiza watu wote wafurahi na mwaka mpya, wale vizuri, wavae nguo mpya, wanywe soda na kucheza.

Anasema siku hizi kumaliza mwaka ni kazi ngumu kwa sababu ya matatizo na magonjwa mbalimbali yanayowakabili wanadamu.

Hata hivyo ukiusikiza sana wimbo huu, Kalala amechukua maneno mengi kutoka kwa wimbo wenye maudhui hayo hayo ya 'Tufurahi Kumwaka Mpya' ambao awali ulipigwa kwenye miaka ya '50 na Jean Mwenda Bosco.

**3.Christmas, New Year-Mbaraka Mwinshehe**

Mbaraka Mwinshehe alitunga wimbo wa sikukuu ya krismasi na mwaka mpya, akiwataka watu waende kwenza makanisani wakasali, lakini wakitoka huko wapitie kwenye muziki wa Volcano ambayo ni bendi aliyokuwa akiiongoza.

**4. Christmas, Bonane-King Kiki**

Ni wimbo maarufu sana nchini Tanzania, hasa kinapokaribia kipindi cha sikukuu za krismasi na mwaka mpya.

"Natoka wapi, tukacheze mchezo wa sasa Kamanyola oo, tutoke naye, nakuchukua wangu kipenzi mi waoo hoho.." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo yakiimbwa na Kikumbi Mwanza Mpango King Kiki.

"Ooo Bonane mama" Ni kiitikio cha wimbo huo, wakiwa na maana mwaka mpya.

**5. Krismasi na mwaka mpya-MK Group**

Kwenye miaka ya 90, bendi matata ilivyovuma kwa kipindi kifupi lakini ikitikisa anga la muziki wa Tanzania, MK Group wakiwa na Kasongo Mpinda, walitunga wimbo wa Krisimas na mwaka mpya ambao nao pia ulikuwa ni moja na nyimbo maarufu sana kipindi hiki.




# Celine Dion bado hali mbaya

DADA wa mwanamuziki maarufu wa Marekani, Celine Dion, amesema hali ya msanii huyo inazidi kuleta hofu baada ya baadhi ya misuli kushindwa kufanya kazi.

Claudette Dion amesema hayo wakati akitoa taarifa mpya kuhusu maendeleo ya ndugu yake ambaye anaumwa ugonjwa wa Stiff-Person unaoshambulia misuli.

Akizungumza na jarida la Ufaransa, 7 Jours, alieleza kwa uchungu kuwa mwimbaji huyo wa My Heart Will Go On ameshindwa kujidhibiti baadhi ya viungo kutokana na ugonjwa huo kuendelea kumshambulia.

"Anafanya kazi kwa bidii, lakini hana udhibiti wa misuli yake. Kinachonivunja moyo ni kwamba amekuwa na nidhamu kila wakati katika kazi yake akiwa na imani siku moja atapanda jukwaani," amesema.



## Burna Boy hana ujanja kwa warembo

MWANAMUZIKI nyota kutoka Nigeria, Burna Boy, imeibua mjadala baada ya kumzawadia mpenzi wake wa zamani Stefflon Don, gari la kifahari kama zawadi.

Video ya gari hilo imesambaa katika mitandao ya kijamii na kuibua hisia kwa mashabiki wa muziki kuwa wawili hao wamerudisha uhusiano wao wa kimapenzi baada ya kuachana muda mrefu.

Stefflon Don ambaye ni rapa kutoka nchini Jamaica, ambaye anaishi Uingereza, amepewa zawadi ya gari hilo aina ya Rolls Royce kama zawadi ya siku yake ya kuzaliwa.


## Vin Diesel akabiliwa na mazito


MWIGIZAJI mkongwe wa filamu za Hollywood, Vin Diesel anakabiliwa na mashtaka ya unyanyasaji wa kingono kutoka kwa msaidizi wake wa zamani.

Asta Jonasson amelalamika kuwa amefanyiwa unyanyasaji huo wakati wakirekodi filamu ya Fast Five ya mwaka wa 2010.

Anadai katika kesi hiyo kwamba mwigizaji huyo alimsukuma ukutani huku akijichua.

Aidha anadai baada ya shambulio hilo kampuni yake ilimfukuza kazi na kumsababishia kuwa na msongo wa mawazo.





## Keke Palmer azidiwa kete

MPENZI wa zamani wa mwigizaji wa filamu, Keke Palmer, Darius Jackson amedai katika uhusiano wao amekuwa akinyanyaswa pamoja na kumtukana hadharani.

Kauli hiyo inakuja baada ya miezi kadhaa Palmer kumshutumu Jackson kuwa alimyanyasa na kumnyima haki ya kumlea mtoto wao wa miezi tisa, Leodis.

Kulingana na TMZ, Jackson anadai kuwa Palmer mara kwa mara alifadhaika wakati wa uhusiano wao na alikuwa mkali, hasa baada ya kunywa pombe.

## Tems anamkimbilia Mungu

MWIMBAJI na mtunzi wa nyimbo, Tems amesema mafanikio yake katika muziki yanatokana na mapenzi yake ya kweli kwa Mungu.

Akiwa katika mahojiano na Cool FM, amesema kufanya maombi ni sehemu ya maisha yake ya kila siku hasa anapokuwa njiani.

"Nina mazoea kufanya maombi kila ninapokuwa barabarani, ndani ya ndege au kwenye gari, huwa nasikiliza ujumbe wa aina fulani wa Mungu," amesema.





# Ataka majiko ya gesi vituo watoto yatima

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MJUMBE wa Kamati Kuu (CC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Halima Mamuya, amewashauri wabunge viti maalum mkoani hapa kutoa msaada wa majiko ya gesi kwa vituo vya kulea yatima badala ya wapigakura wao ili viondokane na matumizi ya kuni.

Ushauri huo alitoa jana jijini hapa wakati akikabidhi zawadi za Sikukuu ya Krismasi na fedha za kununulia sare za shule kwa watoto yatima wa kituo cha Karimu.

Mamuya alisema ufike wakati kwa wabunge hao kuona umuhimu wa kugawa majiko hayo kwa makundi makubwa ambayo yanahitaji nishati ya kupikia badala ya kutumia kuni.

"Nadhani njia sahihi badala ya kwenda kugawa majiko ya gesi kwa wapigakura,tuwape hawa wenye uhitaji zaidi," alisema.

Kuhusu bima ya afya kwa watoto, alimshauri Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kurejesha mchakato huo haraka kwa watoto wanaoishi kwenye vituo hivyo baada ya kusitishwa Machi, mwaka huu.

"Watoto walioko katika vituo wanapaswa kushughulikiwa kwa haraka hasa kwenye huduma za matibabu tofauti na watoto wanaopata huduma za matibabu wakiwa nyumbani kwa wazazi au walezi wao. Kwa sababu hii ninaomba sana Ummy aharakishe kwa sababu kuna watoto wapo vituoni na wanahitaji matibabu kila siku," alisema.

Mamuya aliahidi kuwasilisha kilio hicho kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na viongozi wengine ili kuwasaidia watoto yatima ambao idadi yao ni kubwa kwa kuwa serikali pekee haiwezi kuwalea.

Kuhusu ubovu wa barabara ya kwenda kwenye kituo hicho cha Karim, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Arusha, Wilfred Soileli, alisema atawasiliana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili ifanyiwe matengenezo na kupitika kwa mwaka mzima.

Awali Ofisa Ustawi wa Jamii, anayeratibu Dawati la Familia, Evonoia Kikavo, alisema watoto wanaoishi kwenye vituo wanakabiliwa na ukosefu wa huduma za matibabu.

# Watu 37 wagundulika na matatizo ya moyo

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WATU 37 wamegundulika kuwa na magonjwa ya moyo baada ya kufanyiwa uchunguzi na madaktari bingwa wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro.

Watu hao ni kati ya 307 waliojitokeza kufanyiwa uchunguzi wa moyo na madaktari katika kambi maalumu ya siku tano iliyowekwa wilayani hapa kuanzia Desemba 18 hadi 22, mwaka huu .

Kutokana na takwimu hizo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, ambaye pia ni Mbunge wa Siha, amesema Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge ameridhia kuongezwa siku mbili zaidi za uchunguzi wa magonjwa hayo kwa wakazi wa wilaya hiyo na za jirani.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa uchunguzi na matibabu ya moyo katika Hospitali ya Wilaya ya Siha, Dk. Mollel, alisema amelazimika kuzungumza na Dk. Kisenge kuhusu uhitaji huo na kukubali kambi hiyo kusogezwa hadi Desemba 24, mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Christopher Timbuka, alisema kambi hiyo imewasaidia wakazi wa wilaya hiyo na za jirani kuchunguzwa afya zao.

"Watu waliokutwa na changamoto zinahitaji referral (rufani) ya haraka. Na hii huduma kama isingekuwepo ingewachukua wagonjwa muda mrefu sana kuifikia JKCI," alisema na kuongeza: "Tungeweza kupoteza watu wengi, lakini kutokana na kuja kufanyiwa vipimo hapa, watu wamepata hii huduma vizuri na bila gharama," alisema.

Mkurugenzi wa Tiba Shirikishi na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa JKCI, Dk. Delila Kimambo, alisema taasisi hiyo imeweka kambi Siha kwa ajili ya upimaji wa magonjwa hayo ya moyo kwa watoto na watu wazima.

"Hii ni mojawapo ya huduma inatolewa na taasisi yetu ambayo inaitwa 'Dk. Samia Suluhu Hassan Tiba Mkoba' maana yake tunawafuata wananchi pale waliko kwa ajili ya kufanya vipimo vya moyo, kuongeza ujuzi kwa madaktari, kutoa nafasi ya kugundua matatizo ya moyo kwa watu ambao wasingeweza kupata nafasi ya kufika kwenye taasisi yetu na mapema," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kimambo, tangu waanze kambi hiyo Disemba 18 mpaka 21 wamewafanyia uchunguzi watu hao 307 na kubaini magonjwa yanayoongoza kuwa ni shinikizo la damu, ikifuatiwa na mishipa ya moyo kuziba, matatizo ya mbavu na ya moyo kwa watoto wanaozaliwa wakiwa na matundu kwenye kiungo hicho.

"Wagonjwa 37 waliogundulíwa kuugua magonjwa ya moyo wanahitaji uchunguzi zaidi na hawa watafuata taratibu na kupewa rufani kwenda Hospitali ya Magonjwa ya Moyo ya Jakaya Kikwete kwa huduma zaidi," alisisitiza.



Diwani wa kata ya Majengo wilayani Muheza Tanga, Mukadam Sabuni akizungumza na wananchi wa kata hiyo juzi katika mkutano wa hadhara wa kuzungumzia mambo mbalimbali ikiwemo miradi iliyofanyika katika uongozi wake uliofanyika Majengo shimoni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ofisa elimu, mhandisi wa jiji matatani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

OFISA Elimu wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Joshua Mange na Mhandisi wa Jiji hilo, Jacob Mwakiambiki wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za uzembe katika utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa shule mpya ya sekondari Murieti.

Kushikiliwa kwa watuhumishi hao na jeshi hilo kunatokana na agizo la Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongela baada ya kukagua ujenzi wa mradi huo na kubaini kuwapo kwa dosari mbalimbali.

Kwa mujibu wa Mongela, ofisa elimu huyo, anakabiliwa na tuhuma za kushindwa kubaini meza za zege kwenye maabara ya masomo ya sayansi imejengwa kinyume na taratibu.

Mwakiambiki anakabiliwa na tuhuma za kushindwa kumsimamia fundi jamii aliyepewa zabuni ya ujenzi huo.

Vilevile Mongella ameagiza fundi huyo, Chanzala Said kukamatwa na kuwekwa mahabusu kwa tuhuma za kujenga maabara hiyo chini ya kiwango, kuvuja, kutokamilisha mfumo wa miundombinu ya maji, hasa kwenye vyoo.

"Hivi Mkurugenzi, hebu angalia vitu vilivyokuwa hovyo hovyo, jengo linavuja na limechakaa hata kabla ya kukamilika mnapokujaga huku kukagua mnakaguaga nini?" Alihoji.

"OCS (Mkuu wa Kituo cha Polisi), hebu chambuachambua wahusika walioko hapa, uangalie wa kuondoka nao na wasipewe dhamana hadi mimi nitakaporuhusu," alisema.

Alisema kama mkuu wa mkoa, amemepewa jukumu la kutafuta suluhisho la matatizo yanayowakabili wakazi wa Arusha na sio kushiriki kwenye michakato na mijadala yao.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Enzi ambazo Challenge Cup ilikuwa na msisimko kama Kombe la Dunia

**Na Adam Fungamwango**



Kikosi cha timu ya soka ya taifa ya Tanzania Bara, kilichoshiriki Kombe la Afrika Mashariki na Kati, CECAFA Challenge mjini Nairobi, Kenya mwezi Novemba, mwaka 1979 Kutoka kulia waliosimama ni Salim Amir, Jellah Mtagwa, Athumani Mambosasa (marehemu), Juma Mkambi 'Jenerali' (marehemu), Mohamed Salim, Peter Tino na kocha, Joel Bendera (marehemu). Waliochuchumaa kutoka kulia ni Daudi Salum 'Bruce Lee', Omar Hussein 'Keegan', Mohammed 'Adolph' Rishard, Hussein Ngulungu na Mohamed Kajole (sasa marehemu).

KWA sasa limekosa mvuto na halina msisimko tena kama ilivyokuwa zamani miaka ya mwanzoni mwa 1980, hadi katikati ya miaka ya 1990. Nalizungumzia Kombe la Challenge. Ni kombe linaloshirikisha timu za taifa kutoka nchi za Afrika mashariki na kati.

Kwa miaka ya karibuni lilionekana kubadilika na kuzishirikisha zaidi nchi za Ukanda wa CECAFA, kukiwa pia na ongezeko la nchi kama, Burundi, Rwanda, Somalia, Sudan Kusini, Eritriea na nyinginezo.

Miaka ambayo Kombe la Challenge liliwateka mashabiki wa soka nchini vilivyo ilizishirikisha hizo nchi nilizozitaja mwanzo hazikuwepo na badala yake kulikuwa na nchi ambazo kwa sasa hazichezi kwenye michuano hiyo na hata kama ikitokea moja, basi itakuwa imealikwa tu.

Nchi hizo ni Zambia, Malawi na Zimbabwe. Kombe hili lilianzishwa na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati.

Hapa Tanzania michuano hiyo inapofanyika nchi yoyote ile, basi mashabiki wa soka walikuwa wanaifuatilia kupitia redio ya taifa, Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

Iwe inafanyika nchini au nchi yoyote, mtangazaji au watangazaji wataambatana na timu kwenda kutangaza moja kwa moja michuano hiyo.

Na zilikuwa zinatangazwa mechi zote. Kwa sababu nchini hakukuwa na teknolojia ya televisheni au mitandao, Watanzania walikuwa wakiifuatilia kupitia redio zao tu.

Kombe la Challenge kwa Wabongo miaka hiyo lilikuwa maarufu zaidi kuliko hata Kombe la Dunia ambayo matokeo ya mechi yanakuja kujulikana siku tatu baada ya mechi kuchezwa kwa kutangazwa na RTD. Si kama hivi sasa ambapo inaonekana laivu kwenye televisheni mechi ya kwanza hadi fainali.

Kutokana na michuano hii kupendwa na kufuatiliwa sana na Watanzania wengi miaka hiyo, hadi leo hii kuna majina ya wachezaji wa timu za nchi zilizokuwa zinashiriki michuano hiyo hayatosahaulika. Si wote, bali wale waliokuwa mahiri na mastaa sana wakati huo.

Ndiyo maana hadi leo Watanzani hawajawasahau wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia waliofariki kwa ajali ya ndege Aprili 27, 1993 pwani ya Gabon walipokuwa wakienda kucheza mechi ya kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia dhidi ya Senegal.

Ni kwa sababu mwaka mmoja uliopita wakifika nchini Tanzania kucheza Kombe la Challenge na kufanya vema, ikiacha gumzo kubwa kutokana na kuwa na wachezaji mahiri. Ilishika nafasi ya tatu kwa kuifunga Malawi mabao 4-0, huku Uganda ikitwaa ubingwa kwa kukichapa kikosi cha pili cha Taifa Stars kilichojulikana kama Kakakuona bao 1-0.

Ndiyo maana Watanzania waliwalilia sana kina Efford Chabala, John Soko, Whiteson Changwe, Robert Watikayeni, Eston Mulenga, Derby Makinka, Moses Chikwalakwala, Wisdom Mumba Chansa, Kelvin Mutale, Numba Mwila, Patrick Banda, Kenan Simambe, Timothy Mwitwa, Richard Mwanza, Moses Masua na wengineo.

Timu ya taifa ya Zambia siku zote wapinzani wao wakubwa walikuwa na Malawi. Nao kwenye miaka ya 1980 nhadi katikati ya 1990 walikuwa na wachezaji waliondokea kuwa maarufu.

Nao ni Jonathan Bilie, Jack Chamangwana, Young Chimodzi, Stocker Danzide, Clement Mkwalula, Jimmy Mfamba, Clifton Msiya, Frank Sinaro, Collin Thewe, Hlman Malunga, Lawrence Wala na ndugu yake Harry Waya.

Timu ya taifa za Zimbabwe ilikuwa na wachezaji kama Mosses Chunga, Shacky Tauro, Stanley Ndunduma, Oliver Kateya na wengineo.

Harambee Stars, timu ya taifa ya Kenya ilikuwa na wachezaji mahiri kama Mahmoud Abbas, Elly Adero, JJ Masiga, Peter Otieno Basanga, James Ouma, Josephat Murila, Nashon Mahila, Sammy Tabu, Bob Ogola, Hussein Kheri, Ambroce Ayoyi na Wilbaforce Mulamba.

Uganda nayo haikuwa nyuma, kwani ilikuwa na wachezaji wasiosahaulika, kina Paul Hasule, Godrey Kateregа, Godfrey Higenyi, John Latigo, Fred Mukasa, Paul Nkata, Phillip Omondi, Issa Ssekatawa, Adam Ssemugabi, Majid Musisi na Jackson Mayanja.



Kikosi cha timu ya taifa ya Kenya, Harambee Stars kikiwa kwenye Uwanja wa Taifa Dar es Salaam (sasa Uhuru) kabla ya kucheza fainali ya Kombe la Challenge mwaka 1981 dhidi ya Taifa Stars na kushinda bao 1-0 kikiondoka na kombe nchini. Waliosimama kutoka kushoto ni Apollo Ndeda, Mahmoud Abbas, Tony Lidonde, Peter Otieno, Josphat Murila, Avedi Mjumbe, Bobby Ogolla, Jack Sihul, Elly Adero, na Apollo Obota Waliochuchumaa kutoka kushoto ni Jared Ingutia, Wilberforce Mulamba, Haggai Mirikau, Ambrose Ayoyi, Hussein Kheri, James Ouma, Sammy Taabu.

# Waziri akamatwa kwa ufisadi Kenya

**NAIROBI,** KENYA

WAZIRI wa zamani wa Utalii nchini Kenya, Najib Balala, amekamatwa kwa tuhuma ya kufanya ufisadi akiwa madarakani.

Kulingana na vyombo vya habari nchini humo, maofisa wa upelelezi wa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi(EACC) walimkamata Balala na wenzake watatu kwa ajili ya kufanyiwa mahojiano.

Hatua hiyo inafuatia madai kuwa hazina ya utalii ililipa kwa ulaghai shilingi za Kenya bilioni 8.5 ili kuanzisha Chuo cha Utalii tawi la Pwani wakati huo akiwa waziri.

Balala alikamatwa pamoja na watu wengine akiwemo Leah Adda Gwiyo, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii, na Joseph Odero aliyekuwa mhandisi wa kampuni ya West Consult Engineers.

EACC ilifanya uchunguzi kuhusiana na malipo hayo na kuwasilisha ripoti ya uchunguzi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma ambaye alikubaliana na mapendekezo ya kukamatwa na kuwafungulia mashtaka watu 16.

Washukiwa hao wanakabiliwa na makosa 10 ya ufisadi na uhujumu uchumi.

Washukiwa hao hawajazungumza lolote kuhusu tuhuma zinazowakabili

Msemaji wa Tume hiyo, Eric Ngumbi alinukuliwa na vyombo vya habari akisema Balala atasafirishwa kutoka Nairobi hadi Mombasa ambako atafikishwa katika mahakama ya Malindi kujibu mshtaka yake.

**BBC**

# Matokeo ya urais DRC kuanza kutangazwa leo

**KINSHASA,** DRC

MATOKEO ya uchaguzi mkuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) yanatarajiwa kuanza kutangazwa leo, licha ya wagombea wa upinzani kulalamikia zoezi hilo kufanyika katika hali ya vurugu na ucheleweshaji wa vifaa katika vituo vya upigaji kura.

Uchaguzi ulimalizika Alhamisi jioni baada ya siku mbili za upigaji kura kutokana na kujitokeza kwa changamoto mbalimbali ikiwamo matatizo ya vifaa ambayo yalisababisha vituo vya kupigia kura katika mikoa mbalimbali kutofunguliwa Jumatano ambayo ilitengwa siku maalumu ya uchaguzi.

Tume ya Uchaguzi nchini humo (CENI) iliongeza siku ya kupiga kura hadi Alhamisi baadhi ya vituo vya kupigia kura, lakini mpaka jioni kulikuwa na msururu wa wapiga kura wakisubiri kutimiza haki yao. Tume hiyo ilitangaza matokeo ya kwanza yanatarajiwa kutolewa leo kwa nafasi ya urais.Rais anayemaliza muda wake, Felix Tshisekedi, anawania muhula wa pili na kupewa upinzani na wagombea wengine 18, wakiwamo Moise Katumbi ambaye alikuwa gavana wa jimbo la Katanga. Uchaguzi ho ulifanyika katika nafasi mbalimbali ikiwa ni pamoja na urais, ubunge na magavana na serikali za mitaa.

Hata hivyo, imekuwa vigumu kukadiria ni vituo vingapi kati ya 75,000, vilivyoongezewa muda wa kupiga kura vilimaliza kwa usalama hadi jioni wakati muda huo ulipomalizika.

Idadi kubwa ya vituo vilivyoathirika vilikuwa katika vijiji ambavyo ni vigumu kufikiwa, na katika miji mikubwa kama Kinshasa, Lubumbashi na Goma.

Wakati huo huo, Baraza la Maaskofu nchini DRC(CENCO) na Kanisa la Kristo nchini Congo (ECC) umetoa tathmini zao za uchaguzi na kueleza kulikuwa na kasoro nyingi.

Walisema asilimia 16 ya mashine za kupigia kura zilizowekwa katika vituo maalum kwenye majengo ya shule, kambi za jeshi na nyumba za ibada havijatolewa.

Ujumbe huo wa CENCO-ECC uliongeza kwamba karibu asilimia 65 ya malalamiko ya wapiga kura hayakututatuliwa kwa mpigakura wa kwanza katika kila kituo.

**RFI**



Wagonjwa wakiwa wamelala chini bila kupata huduma za matibabu katika moja ya hospitali iliyoko Ukanda wa Gaza.
**PICHA: REUTERS**

# Hamas yasisitiza haitawaachilia mateka

**GAZA,** PALESTINA

KUNDI la Hamas ambalo linadhibiti Ukanda wa Gaza, limesema hawatawaachilia mateka wanaowashikilia hadi Israel itakapokubali kusitisha mashambulizi yake kabisa.

Wakati kauli hiyo ikitolewa, Jeshi la Israel lilitangaza kuwaua wapiganaji 2,000 wa Hamas katika operesheni yake ya kivita inayoendelea Gaza.

Jeshi hilo lilisema takwimu hiyo ni tangu kuanza usitishwaji wa mapigano mapema mwezi huu wakati mateka zaidi ya 100 waliachiliwa.

Watu 120 waliotekwa nyara kutoka ndani ya Israel Oktoba 7, wanaaminika kuwa bado wanashikiliwa mateka katika maficho Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo, juhudi zinaendelea kufanywa na Umoja wa Mataifa kupitisha azimio kuhusu kusitishwa kwa vita kati ya pande mbili zinazopigana.

Serikali ya Marekani ilisema bado ina wasi wasi kuhusu rasimu ya azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, na kusababisha upigajikura kuahirishwa na ungefanyika jana.

Huko Ukanda wa Gaza, mapigano makali yanaendelea, huku Israel ikishambulia kwa kutupa mabomu kaskazini na kusini mwa eneo hilo na Hamas wakirusha makombora kuelekea mjini Tel Aviv.

Miongoni mwa Wapalestina walioripotiwa kuuawa ni mkurugenzi wa kituo cha polisi katika mji wa kusini wa Khan Younis na binti wa Waziri wa Afya wa Gaza.

Katika makubaliano yaliyodumu wiki moja, yaliongeza upelekaji wa misaada ya kibinadamu ndani ya Gaza na kurejesha utulivu ka muda.

Aidha, Umoja wa Mataifa umeonya kwamba watu wako katika hatari ya kukabiliwa na baa la njaa ikiwa vita kati ya Israel na Hamas vitaendelea.

Mazungumzo kuhusu mapatano mapya yanafanyika mjini Cairo nchini Misri, ingawa awali hapakuwa na makubaliano yoyote.

Katika taarifa iliyotolewa na Hamas ilisema kuna uamuzi wa kitaifa wa Palestina kwamba kusiwe na mazungumzo kuhusu wafungwa au kubadilishana mikataba isipokuwa baada ya kusitishwa kabisa kwa uchokozi.

Islamic Jihad, kundi dogo katika Ukanda wa Gaza, ni miongoni mwa wanaojulikana kuwashikilia mateka wa Israel.

Kauli hiyo ya Hamas inaiweka serikali ya Israel katika wakati mgumu baada ya mpango wake wa kutumia nguvu kushinikiza kuachiliwa mateka kushindikana.

Serikali ilisema inafikiri njia bora ya kuachiliwa kwa mateka hao ni kuweka shinikizo la kijeshi dhidi ya Hamas na pia kuandaa shughuli za uokoaji.

**BBC**

# HABARI PICHANI



Watuhumiwa wa kesi ya uhujumu Uchumi kwa kusafirisha dawa za kulevya, wakienda katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana kusomewa maelezo ya mashahidi na vielelezo katika kesi yao. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Katibu Tawala wilaya ya Muheza Tanga Mohamed Mfaki (kushoto) akizungumza na mkuu wa kikosi Polisi wa Usalama Barabarani wilayani Muheza, Leonard Bandola juzi baada ya kumalizika kikao na madereva wa pikipiki maarufu bodaboda kilichowakutanisha vyombo vya LATRA na jeshi la polisi usalama barabarani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Wajasiriamali katika Manispaa ya Shinyanga wakiwa kwenye mkutano wa kupewa elimu ya ujasiriamali na fursa zilizopo ili wazichangamkie na kujikwamua kiuchumi pamoja na kupata mikopo isiyo na riba ya halmashauri asilimia 10 ambayo asilimia 4 hutolewa kwa vijana na wanawake na asilimia 2 watu wenye ulemavu. **PICHA: MARCO MADUHU**



Naibu Waziri wa Afya ambaye pia ni Mbunge wa Siha Dk. Godwin Mollel (kulia) akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Siha Dk Christopher Timbuka funguo za gari moja kati ya matatu yaliyotolewa na Serikali kwa wilaya hiyo ambalo litatumika katika huduma za afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkurugenzi wa shule ya awali na msingi Glisten ya Mji mdogo wa Mirerani Wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Justin Nyari akiwapongeza wanafunzi, walimu na wazazi, **PICHA: GIFT THADEY**

# HADITHI

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba.

Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu.

Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

# Mama mwenye nyumba-7

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Mume wa Devota aliomba msamaha na kukaa kimya. Mkewe alikuwa na mawazo tofauti kidogo, lakini kwa mbali ni kama yaliendana.

Wala hawakukutana kwa ajili ya kutengeneza mahusiano. Na wala hakutaka kumfafanulia kwa sababu ilikuwa ni kuuwasha moto mwingine.

Akakumbuka maongezi waliyokuwa wakiongea siku hiyo, hasa yale aliyoongea mama mwenye nyumba.

"Baba nakwambia, mimi sina ugomvi na wewe, lakini yule mke wako anaweza kusababisha nikawahamisha kabisa ndani mle.

"Mkeo ananitolea mimi mineno ya shombo. Mkeo hataki kufanya usafi, kweli. Nikisema mtasema mwenye nyumba ana mdomo.

"Na mwanamke yule wewe umemuokota wapi? Mwanaume mzuri, mtanashati kama wewe wa kwenda kuwa na kijanamke chenyewe chembambamba kama kinakula simenti, chini miguu kama fito za kujengea nyumba ya udongo, haya mtu mwembamba, lakini miziwa mama miziwa, he we baba..

Ndiyo bwana wewe, sasa hivi kwa jinsi ulivyo unatakiwa uwe na japo mwanamke mwingine pembeni akupetipeti."

"Nakupa binti yangu wa kwanza. Ndiyo, binti mbichi kama yule atakuwa sawa na limama lako lile?" Ni baadhi ya maongezi ambayo waliyaongea kule. Mume wa Devota akili ikamwambia tu kuwa kama angesikia hiki kilichoongelewa, moto ungewaka.

"Kwanza wewe mume wangu unanidhalilisha sana! Unakwendaje kusimama na mwanamke ambaye mashavu yanachuma kunde? Mama huyu mtu mzima wewe utampeleka wapi? Au kakwambia utakuwa wewe ndiyo baba mwenye nyumba na kijumba chake kibovu hiki?" Maneno yalizidi kumtoka Devota.

"Basi mke wangu, mimi nimeshakwambia yaishe, yeye alinifuata tu kwa ajili ya kuniambia matatizo ya hapa ndani, lakini siyo kama tuna mahusiano!"

"We haya tu, hivi huoni kama aibu kuchukua mama mtu mzima mwenye ngozi kama taulo..."

"Sasa mke wangu hebu basi ongea taratibu, atasikia halafu itakuwa matatizo..."

"Kusikia, asikie mwanaharamu mkubwa, kazi kuchukua waume za watu, kisa kichumba chake kibovu cha urithi."

Mume wa Devota akaona bora anyamaze tu, maana mkewe ameshapandwa na munkari, atakapokuwa anamjibu au kuongea na yeye mwisho Mwantumu atasikia, halafu itakuwa ni kama kuwasha njiti ya kibiriti karibuni na kituo cha mafuta.

Akamuacha aendelee, kwani ni bora uongo huu alionao, kuliko ukweli wa jambo halisi ambalo angelijua.




**"Haya haya, hapa kuna mchango wa buku buku tukaweke umeme. Haiwezekani tulale giza, kila chumba kinatakiwa kitoe elfu moja ili tumalizie hizi siku mbili tatu kabla mwezi haujaisha ili tuchange tena elfu kumi kumi." Ni sauti ya mama mwenye nyumba akiwaambia wapangaji wake.**

******************************

"Haya haya, hapa kuna mchango wa buku buku tukaweke umeme. Haiwezekani tulale giza, kila chumba kinatakiwa kitoe elfu moja ili tumalizie hizi siku mbili tatu kabla mwezi haujaisha ili tuchange tena elfu kumi kumi." Ni sauti ya mama mwenye nyumba akiwaambia wapangaji wake.

Ilikuwa saa 12:00 jioni hivi umeme ulipokatika kwenye nyumba hiyo. Awali ilidhaniwa kuwa ni mgao.

Baada ya uchunguzi wa muda mfupi kwa kusikia nyumba za jirani muziki unaendelea kudunda, wakajua kuwa ni Luku.

"Jamani kwani humu ndani kuna watu hawatumii umeme? Mbona hawalipi. Kama inapigwa donesheni ya buku buku leo na mama mwenye nyumba lazima atoe na yeye, tunatoa sisi tu yeye mbona hatoi, au kwa sababu ndiyo mwenye nyumba?" Ni dongo kutoka kwa Rozi kuelekea kwa mama mwenye nyumba.

"We mtoto koma, mimi siyo saizi yako ongea kwa adabu.."

"Ndiyo tunasema, sasa tukasemee wapi? Hizo shilingi elfu kumi kumi huwa tunatoa sisi tu, wewe hatujakuona hata siku moja unatoa, na wewe ndiyo peke yako ndani una friji." Rozi alimpasha.

"Toa basi mama mwenye nyumba na sisi tutoe." Tabia aliingia kati.

"Wewe nawe ndiyo usiseme kitu kabisa, mbea mkubwa we."

"Siyo umbea, si tumeambiwa tutoe pesa, sasa kwa nini tusihoji? Tutatoaje peke yetu! Na wewe leo mama mwenye nyumba tusaidie."

"Wewe unanitafuta muda mrefu, juzi nimekuona unaingia chumbani kwa huyu kikaragosi mwenzako, ukaenda kumwambia kuwa eti mimi ndiyo nilificha ufagio wake."

Tabia akamwangalia Mwantumu halafu akamjibu." Ndiyo kweli nilimwambia, sasa tufiche kwani uchawi, nimekuona kwa macho yangu haya mawili, umetoka ndani kwa kunyata, ukaurudisha pale uwanjani."

Maneno hayo yalimfanya mama mwenye nyumba kupata hasira ya ghafla.

"Unasemaje wewe? Mimi ndiyo niliyeiba fagio?"

"Sijasema umeiba, umeficha, nimekuona!" Tabia akajibu kwa uhakika zaidi.

Mwantumu akafura na ghfla kwa kasi ya ajabu alimfuata Tabia alipo. Na yeye pia alikuwa akisubiriwa kwa hamu na mwenzake.

Devota na Rozi hawakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuamulia. Wakavaana na kuangushana chini.

Wakati kila mmoja akijipapatua angalia kumpiga mwenzake ngumu moja, walijikuta waliinuliwa kwa nguvu na kuachanishwa.

"Nakwambia leo utahama, natoa vyombo vyako nje." Mama mwenye nyumba aliongea kwa sauti ya hasira.

"We we we, bila pesa yangu patachimbika bila jembe hapa nakwambia, nirudishie pesa yangu iliyobaki ya kodi, naondoka mwenyewe." Tabia akamjibu Mwantimu.

Ni muda huo huo ambao aliingia mjumbe wa nyumba kumi ambaye alikwenda kuitwa na wapambe.

Kikawekwa kikao cha dharura ambacho kilichoamriwa ni kwamba wapangaji wote wahame.

"Nyumba hii nasikia kila siku ugomvi, sasa amri imetoka serikali za mitaa, wapangaji wote kodi ikiisha waondoke," akasema mjumbe.

"Mjumbe hata sisi yametufika hapa, hatuwezi kuendelea tena kukaa na huyu mama, tangu aje hapa ni kivumbi na jasho. Hata wenyewe hapa tumeshachoka, bila hata kutuambia kila mmoja mkataba wake ukiisha anaondoka na tayari tumeshaanza kutafuta vyumba," Devota alimwambia mjumbe halafu akaongeza.

"Lakini mwambie huyo mama hata sisi tukiondoka, akiendelea na tabia yake hiyo ya ukorofi, umbea, upekepeke, uongo na kutaka kuchukua waume za watu, hawezi kukaa mpangaji yoyote yule..."

"Unaona mjumbe, hayo ya kuchukua waume za watu yametokea wapi?" Mwantumu alisimama ghafla kikaoni.

ITAENDELEA JUMAPILI

HABARI MICHEZO

# KABURU: SIMBA ITABEBA TAJI LA LIGI YA MABINGWA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Baraza la Ushauri la Simba likizinduliwa rasmi juzi, Mjumbe wa baraza hilo, Geoffrey Nyange 'Kaburu' amesema anaamini timu yao ni bora na itafanya 'mambo ya kutisha' ikiwamo kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wajumbe 21 waliteuliwa kuunda baraza hilo ambalo mwenyekiti wake ni Jaji Mstaafu, Thomas Mihayo, lengo lake ni kushauri uongozi wa Simba kufikia mafanikio.

Akizungumza mara baada ya kikao hicho, Kaburu, alisema ingawa wamekutana kwa mara ya kwanza lakini kikao kiliendа vyema na mikakati ya kuijenga Simba mpya, bora na yenye mafanikio, ndani na nje ya nchi ulianza.

"Tumezindua leo (juzi) baraza letu la ushauri la klabu ya Simba, limepata nafasi ya kukutana na viongozi wetu ambao tumewahi kufanya kazi pamoja huko nyuma, kwa hiyo naamini ni mwanzo mzuri wa kuwa na Simba bora zaidi.

Niseme nia ni njema kwa waliofikiri na kuja na haya maamuzi, nimshukuru sana mwekezaji wetu Dewji (Mo), Bodi ya Wakurugenzi, pamoja na wadhamini wetu kwa kuja na hili jambo, sisi lengo letu sio tu kufika robo fainali, lakini tunafika fainali na hatimaye siku moja kulichua Kombe la Afrika, naamini kwa uzoefu, na ushirikiano huu wa pamoja wa Baraza la Ushauri na Bodi, wanachama na mashabiki, naamini tunakwenda kufanya jambo kubwa zaidi," alisema Kaburu.

Aliongeza wanafahamu soka la sasa lina ushindani na hakuna tena timu ndogo huku kwao wamejipanga kujiimarisha kwa sababu kila mechi ni fainali.

Wajumbe wengine wanaounda baraza hilo ni pamoja na Ismail Aden Rage, Hassan Dalali, Azim Dewji, Kassim Dewji, Swedi Nkwabi, Evans Aveva, Mwina Kaduguda, Farough Baghouza, Musleh Al-Ruweh, Mohamed Nassor, Mulamu Ng'ambi na Octavian Mshiu.

Wengine ni Profesa Mohamed Janabi, Hassan Kipusi, Gerald Yambi, Moses Kaluwa, Crescentius Magori na Idd Kajuna.

Katika hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba iliyoko Kundi B iko katika nafasi ya pili ikiwa na pointi tano huku vinara wa kundi hilo wakiwa ni ASEC Mimosas yenye pointi 10.




Mwanafunzi wa Chuo cha Mzumbe, Ayoub Mwenda (katikati) akipokea vifaa vya umeme kutoka kwa Meneja wa Tigo Kanda ya Pwani, Gwamaka Mwakilembe (kulia), baada ya kushinda zawadi ya Magifti Dabodabo inayoendeshwa na kampuni hiyo. Kushoto ni mshindi mwenza, Selemani Omary. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashujaa yaiendea Simba Dodoma

**Na Saada Akida**

ILI kujiimarisha kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba, kikosi cha Mashujaa FC kimeweka kambi yake jijini, Dodoma, imeelezwa.

Mashujaa wanatarajia kuwakaribisha Wekundu wa Msimbazi Desemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Mashujaa, Hussein Bunu, alisema kwa sasa timu yao imeweka kambi Dodoma kujiandaa na mchezo huo ambao wanaamini utakuwa na ushindani kwa pande zote mbili.

Bunu alisema wanatarajia kucheza kwa tahadhari katika mchezo huo ili kufikia malengo yao ya kuvuna alama tatu muhimu kutoka kwa wageni hao.

"Maandalizi yetu yanaendelea vizuri, tunajiandaa kuikabili Simba, tunatambua ubora wao na kocha wetu Bares (Abdallah Mohammed) ameshaanza kusahihisha makosa tuliyoyafanya katika michezo iliyopita ili kutojirudia kwenye mchezo huo. Tunatambua ubora wa Simba, wana wachezaji wazuri na wazoefu," alisema Bunu.

Aliongeza kutokana na walivyoiona Simba hivi karibuni, wameamua kutafuta mazingira mazuri yenye utulivu ili kukiandaa vyema kiufundi, kimbinu na kisaikolojia, tunataka wachezaji wetu wawe tayari kupambana kufikia malengo," Bunu alisema.

Aliongeza wanataka kuona wanautumia vyema uwanja wa nyumbani na kubwa ni kuwapa furaha mashabiki wao.

## Chabruma afunguka wanawake wameiva

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuanza na ushindi, Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, amesema msimu wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake 2023/2024 hautakuwa rahisi kwa sababu kila timu imejipanga na imejiimarisha kusaka matokeo chanya.

Mabingwa hao watetezi, JKT Queens walianza msimu mpya ugenini na kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya wenyeji, Bunda Queens.

Chabruma alisema kuwa timu yake ilikutana na ushindani kutoka kwa wenyeji licha ya kushiriki kwa mara ya kwanza katika ligi hiyo ya juu ya wanawake hapa nchini.

"Msimu huu hautakuwa rahisi kwa sababu timu zote zimejipanga vizuri, zimefanya usajili mzuri, ukiwaangalia hawa Bunda Queens tuliwazidi uzoefu na kutumia makosa yao kupata ushindi. Sasa tumemalizana na Bunda Queens na tunajipanga kwa mechi yetu inayofuata dhidi ya Geita Gold Queens," alisema kocha huyo.

Aliongeza mipango yao ni kuhakikisha wanafanikiwa kuvuna pointi tatu katika kila mechi watakayocheza ili kutetea ubingwa wanaoushikilia.

## Kitambi aing'arisha Geita Gold Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Denis Kitambi juzi ameiongoza Geita Gold kupata ushindi wake wa kwanza tangu ajiunge na timu hiyo wiki hii akitokea Namungo FC, baada ya kuichapa Singida Fountain Gate bao 1-0, mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mwenyewe akisema kazi ndio imeanza.

Kitambi alitua Geita Gold kuchukua nafasi ya Hemed Suleiman 'Morocco' ambaye amekuwa na majukumu mengi zaidi katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

"Ni muda mfupi tu nimeingia katika timu, nadhani ni mwanzo mzuri, ushindi huu utawafanya wachezaji waendelee kujiamini na nitaendelea kuingiza vitu vipya taratibu," alisema Kitambi.

Bao la Valentino Mashaka lililofungwa dakika ya 78 ndio liliwapa Geita Gold pointi tatu muhimu na kuifanya timu hiyo ifikishe pointi 16 na imechupa hadi nafasi ya 10 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS SAFI JUVENTUS

JUVENTUS imejadiliana na Manchester City kuhusu mkataba wa mkopo wa kiungo wa England, Kalvin Phillips. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ameiambia City anataka kuondoka katika klabu hiyo mwezi ujao, huku Newcastle United pia ikionyesha nia ya kumnunua kwa mkopo. **(Guardian)**

### INACIO ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inafikiria kutoa pauni milioni 52 kumnunua beki wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Goncalo Inacio, mwenye umri wa miaka 22 ifikapo Januari. **(Sun)**

### CHELSEA: GALLAGHER HAUZWI

CHELSEA haitapokea ombi lolote kutoka kwa Tottenham Hotspur la kutaka kumnunua kiungo wao wa kati, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 23 katika uhamisho wa Januari licha ya kutokuwa na uhakika juu ya hali ya mkataba wake. **(Football Insider)**

### ADARABIOYO KUONDOKA FULHAM

TOSIN Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26 ameiambia Fulham anataka kuondoka katika klabu hiyo msimu ujao kwa uhamisho wa bure. Beki huyo wa zamani wa England amewahi kuzivutia Tottenham Hotspur na Monaco. **(Sun)**

### SPURS KUACHANA NA TODIBO

KLABU YA Tottenham Hotspur itaelekeza darubini yao kwa wachezaji wengine ikiwa hawatampata beki wa Ufaransa na Nice, Jean-Clair Todibo, wiki chache zijazo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 pia amekuwa akihusishwa na tetesi za kuhamia Manchester United. **(Teamtalk)**

### MATIC KUONDOKA RENNES

RENNES iko tayari kuachana na kiungo, Nemanja Matic mwenye umri wa miaka 35 Januari. Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Serbia alijiunga na klabu hiyo ya Ligue 1 kutoka AS Roma msimu uliopita. **(L'Equipe)**

### BARCELONA, MADRID VITANI

BARCELONA na Real Madrid zinaongoza katika mbio za kumsajili, Mason Greenwood, mwenye umri wa miaka 22 na Manchester United kwa sasa hawana mpango wa kumrejesha Old Trafford muda wake wa mkopo utakapomalizika kule Getafe. **(Talk sport)**

### ILING-JUNIOR AGOMBEWA

WINGA wa Juventus na Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 20, Samuel Iling-Junior, ananyatiwa na Tottenham Hotspur, Aston Villa na Brighton. **(Fichajes)**

### JUVE YAMKANA DJALO

KLABU ya Juventus haijakataa kumsajili mlinzi wa zamani wa Ureno, Tiago Djalo, mwenye umri wa miaka 23 kutoka Lille ya Ufaransa Januari, lakini huenda ukafanya hivyo siku za usoni. **(Gazzetta dello Sport)**

### ADAMS SOKONI ENGLAND

WEST Ham na Fulham wanamtaka mshambuliaji wa Nigeria, Akor Adams, mwenye umri wa miaka 23, ambaye huenda akaondoka Montpellier Januari kwa ada ya takriban pauni milioni 15 hadi 20. **(Football Insider)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ERIKSEN ANATARAJIWA KUIBEBA UNITED EPL

Ni baada ya afya yake kuimarika na hivyo kuongeza nguvu...

**MANCHESTER, England**

KIUNGO Christian Eriksen wa Manchester United ana uwezekano mkubwa akawa katika kikosi cha timu hiyo kitakachoshuka kucheza mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya West Ham itakayochezwa leo.

Eriksen alifanya mazoezi na wachezaji wenzake kwa ajili ya kujiandaa na mechi hiyo baada ya United kupambana na kuambulia suluhu dhidi ya Liverpool wikendi iliyopita, huku kiungo huyo akitarajiwa kukipa nguvu kikosi hicho cha Kocha, Erik ten Hag.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 31, alikuwa nje ya dimba tangu kwa kipindi cha wik tano baada ya kuumia kwenye mchezo wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Luton.

Kutokuwepo kwa Eriksen kikosini, United ilipata shida eneo la safu ya kiungo na hivyo kurejea kwake kunatoa uhueni kwa kikosi hicho.

Ikimbukwe United kwa sasa inakabiliwa na majeruhi wengi katika kikosi chake, hivyo kurejea kwa Eriksen kunatoa nafasi ya Tan Hag kuwa na machaguo zaidi.

Wakati huo huo, gwiji wa klabu hiyo, Paul Scholes, anaamini ujio wa Eriksen utaongeza nguvu baada ya mwendo usioridhisha wa timu hiyo katika mechi zao za hivi karibuni.

Akizungumza na kituo cha televisheni cha TNT, Scholes alisema: "Nafikiri Christian Eriksen na Casemiro wakirejea wataongeza nguvu kwenye timu, wachezaji hawa wana uzoefu sana, matumaini yangu wacheze wote, mambo yatakuwa sawa kwa Ten Hag."

Casemiro, Tyrell Malacia na Lisandro Martinez wameondolewa katika kikosi kitakachosafiri kwenda London kwa ajili mchezo huo, huku Harry Maguire, Mason Mount, Victor Lindelof na Amad Diallo pia watakosekana.




# JAMES AFANYIWA UPASUAJI, ATOA 'NENO' WANAOMKASHIFU

**LONDON, England**

NAHODHA wa Chelsea, Reece James alikerwa na kauli mbaya kuhusiana na jeraha lake la hivi karibuni baada ya kufanyiwa upasuaji wa misuli ya paja, juzi.

Beki huyo wa kulia wa England alichechemea katika kipindi cha kwanza wakati Chelsea wakichapwa 2-0 na Everton Desemba 10, mwaka huu kutokana na jeraha la mara kwa mara la misuli wa paja na alifanyiwa upasuaji kujaribu kutatua suala hilo.

Hili ni tatizo la tatu la James tangu mwaka jana, na amesema amekuwa akitumiwa ujumbe mbaya na wa matusi kwake kwenye mitandao ya kijamii.

"Tangu jeraha hili nimekuwa na usaidizi mzuri, lakini kikubwa zaidi ni chuki kutoka kwa baadhi ya watu," aliandika James kwenye Instagram hapo juzi.

"Niamini, sitaki kujeruhiwa, nina furaha zaidi ninapocheza mpira. Lakini wengine wanadhani ni jambo la makusudi."

James aliongeza kuwa, "ahueni yangu imeanza, kimwili na kiakili."

Hata hivyo, sio James mwenyewe wala Chelsea ambao wametoa ratiba ya lini atarejea dimbani.

# Toney kuzikamua Arsenal, Chelsea

**LONDON, England**

KLABU ya Brentford imeziarifu Arsenal na Chelsea kama zinahitaji huduma ya mshambuliaji wake, Ivan Toney, zitatakiwa kulipa kiasi kikubwa cha fedha ili kumnasa katika dirisha Januari au lile la majira ya joto.

Toney mwenye umri wa miaka 27, mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwaka, 2025.

Hata hivyo nyota huyo hajacheza hata mechi moja msimu huu kutokana na majeraha yanayomsumbua.

Brentford inataka kumsainisha



mkataba mpya, lakini bado watamuuza mwisho wa msimu ingawa lazima ofa itakayowasilishwa iwe nono zaidi kwa sababu wanaamini yeye ni mmoja kati ya wachezaji watano bora kwa sasa.

Taarifa za ndani zinaeelza Brentford wanahitaji kiasi kisichopungua cha pauni milioni 80 ili kumuuza.

Mshambuliaji huyo ambaye msimu uliopita alifunga mabao 21 kwenye mechi 25 za michuano yote, Arsenal na Chelsea zinapigana vikumbo kuhakikisha zinanasa saini yake katika dirisha la Januari 2024.

# Saka achangia waathirika Morocco

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Bukayo Saka, amesaidia kujenga Kijji cha Kontena, ambapo waathirika wa tetemeko la ardhi Morocco watakuwa wakiishi.

Winga huyo wa kimataifa wa England, amechangia ujenzi wa makontena 50, sehemu ambayo watu 255 watakuwa wakishi kama makazi yao mapya.

Katika eneo ambalo Saka amesaidia, watu 42 walipoteza maisha, hivyo amejitokeza kusaidia walionusurika akiwa sambamba na mfuko wa hisani wa Big Shoe.

Baada ya kutoa msaada huo, Saka alisema: "Nilishtuka sana niliposikia kuhusu tetemeko la ardhi Morocco.

"Kwa muda ambao tukio limetokea, nilitambua msaada unahitajika haraka, nataka kusaidia watu wa Morocco, nimepata njia ya kuwaisaidia, familia zitapata maeneo mazuri ya kuishi baada ya nyumba zao kubomoka.

"Matumaini yangu familia 84, watoto 89 wataishi kwa amani katika maisha yao ya kila siku."

Makontena hayo yana sehemu ya kulala, jiko, choo na mabafu ya kuogea, pia umeme utapatikana kwa ajili ya matumizi mengine.

Mwaka jana Saka alichangia operesheni ya watoto 120 huko Nigeria ambako ndio asili yake, na hivi karibuni alisapoti waathirika watetemeko la ardhi lilitokea Uturuki.

Saka aliongeza: "Unapoona hali kama hizi watu wanapigania maisha yao, wamepoteza nyumba zao au wapendwa wao, unazidi kutambua unavyoishi wewe ni baraka za Mungu tu.

Saka sio mchezo mkubwa wa soka pekee ambaye amekuwa akisaidia jamii, nyota wa Liverpool, Mohamed Salah amekuwa akichangia fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia nyumbani kwao Misri.



## HABARI MICHEZO

# MANDONGA KUFUNGA MWAKA NA NGUMI YA 'CHIFU KINGALU'

**Na Ashton Balaigwa,MOROGORO**

KUELEKEA pambano lake dhidi ya Mti Jitu, bondia maarufu na mwenye maneno mengi nchini, Karim Mandonga amesema atapamba ulingoni huku akilitambulisha ngumi mpya inayoitwa ,Chifu Kingalu'.

Mandonga anatarajia kupigana na Mti Jitu katika pambano lililopangwa kufanyika Desemba 29, mwaka huu mkoani, Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jana, Mandonga alisema kwa sasa ameamua kuja tofauti na kwa kutumia jina hilo la Chifu Kingalu Mwanabanzi, anaamini atampiga ngumi sehemu yoyote mpinzani wake.

„Bondia Mti Jitu atakutana na ngumi inayoitwa Chifu Kingalu Mwanabanzi, hiyo ngumi imebarikiwa, hiyo ngumi ukitaka mvua inakuja tukiomba jua linakuja, kwa hiyo akae akijua kama Jiti Mawe siku hiyo tutambatiza na kumwita Mama Jiti Mawe, maana atachakazwa na ngumi hiyo" alisema Mandonga.

Naye Mti Jitu alisema hatishwi na vituko vya Mandonga kwa sababu ngumi zake hazimtii hofu na yeye tayari ametumia nguvu ya milima ya Ng'aro, Chamanyani na Mizimu ya Kolelo ili kuibuka na ushindi.

Katibu wa Chama cha Ngumi Mkoa wa Morogoro, Hassan Athuman (Banda), alisema chama hicho kinaendelea kujipanga kuendeleza mabondia vijana ili wapate mafanikio na si kutoa burudani pekee.

Banda alisema wanatarajia kuweka mazingira bora ya kutoa ajira kwa mabondia kupitia ngumi kama ilivyo katika michezo mingine.

Mkurugenzi wa Kimbeho Talents Promotion, waandaaji wa pambano hilo, Majaliwa Kimbeho, ametoa wito kwa wakazi wa Morogoro kujitokea kushuhudia mabondia hao wakipambana lakini pia kupata burudani ya kufunga mwaka.

Kimbeho alisema busara imewaongoza kuwahamasisha vijana wa Morogoro kushiriki katika mchezo huo kutokana na historia ya kufanya vizuri katika tasnia mbalimbali ikiwamo muziki na soka.




Wachezaji wa Azam FC, Feisal Salum (kulia) na Prince Dube (katikati), wakishangilia bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba juzi usiku. Azam ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# Hard Rock yapanga kusajili wapya sita

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WANAJESHI wa Hard Rock FC wamesema wanatarajia kusajili wachezaji sita kutoka katika timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na Zanzibar katika kipindi cha dirisha dogo la usajili ili kuboresha kikosi chao.

Hard Rock inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), yenye makazi yake Kisiwani Pemba ipo katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 17.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Hard Rock, Steve Kapufi, alisema nyota watakaowasajili kutoka nje ya Zanzibar watakuwa ni wachezaji wenye viwango vya juu na uzoefu wa kucheza Ligi Kuu.

Kapufi alisema usajili huo utafanyika kutokana na mapendekezo ya mwalimu anayekinoa kikosi chao lakini pia kulingana na hali ya ushindani uliopo katika ligi hiyo ambayo sasa imepata udhamini.

„Tunataka kusajili wachezaji wazuri na wenye viwango ili kuibakisha timu katika Ligi Kuu Zanzibar, kwa sasa hatuwezi kusema wachezaji gani tutawanasa kutoka Tanzania Bara, muda sahihi utakapofika tutaweka wazi kila kitu," Kapufu alisema.

# Fei Toto, Aziz Ki vitani

INATOKA UK. 24

kirafiki kati ya kikosi cha Bara (Kilimanjaro Stars) dhidi ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), itakayochezwa Desemba 27, mwaka huu.

Mechi hiyo imeandaliwa maalumu kwa ajili ya sherehe za ufunguzi wa Uwanja wa Amaan ulioko Zanzibar ambao umefanyiwa marekebisho chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Idara ya Habari ya TPLB ilizitaja mechi zilizoahirishwa ni kati ya Tabora United dhidi ya Simba, Yanga vs Mashujaa, Mashujaa vs Simba, Kagera Sugar vs Yanga, Simba vs Azam, Geita vs Simba na Yanga dhidi ya Dodoma Jiji iliyopangwa kuchezwa Januari 2, mwakani.

# Simba na Yanga SC majaribuni Ligi Bara

INATOKA UK. 24

muhimu na si vinginevyo.

"Naamini kila mchezaji anatambua ugumu ambao wanakwenda kukutana nao, hivyo kila mmoja tayari amejiandaa kiakili na kimwili kuhakikisha wanakuwa bora," alisema kocha huyo.

Miguel Gamondi, Kocha Mkuu wa Yanga, alisema wataingia kwenye Uwanja wa Jamhuri leo bila kuwadharau wapinzani wao, Tabora United kwa sababu wanahitaji pointi tatu.

Kocha huyo alisema wanahitaji matokeo chanya na ili kufikia mipango yao watashuka dimbani kwa tahadhari.

„Hautakuwa mchezo mwepesi kwa kila timu, nafahamu Tabora United nao watataka kuonyesha ushindani kutafuta pointi, lazima tuwe makini katika dakika zote za mchezo," alisema Gamondi.

Kocha Mkuu wa Tabora United, Goran Kopunovic, alisema wanaifahamu vizuri Yanga na wamejiandaa vyema kukabiliana nao.

„Tupo tayari kukabiliana nao, ni mchezo mgumu lakini tumejiandaa vizuri, tumefanya mazoezi ya kutosha na tupo tayari kutafuta pointi katika mechi hiyo," alisema kocha huyo.

Michezo
Jumamosi Desemba 23, 2023
Nipashe

Eriksen anatarajiwa kuibeba United EPL UKURASA 21



# FEI TOTO, AZIZ KI VITANI

## ●●● Mzanzibar huyo ameendelea kuwa ‚moto' wakati mechi saba zikiahirishwa...



**Na Adam Fungamwango**

BAO alilofunga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba juzi, limemfanya kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum ‚Fei Toto', kufikisha mabao nane na kumkaribia kinara, Stephane Aziz Ki wa Yanga mwenye magoli tisa.

Fei Toto alifunga bao la kwanza dakika ya tisa katika mechi iliyomalizika kwa wageni, Azam FC wakiondoka na ushindi mnono wa mabao 4-0.

Matokeo hayo yaliifanya Azam iendelee kujiimarisha kileleni kwa kufikisha pointi 31 na kufuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 27 huku Simba ikishinda nafasi ya tatu ikiwa na pointi 22, lakini vinara hao wakiwa wamecheza michezo zaidi ya vigogo hao wa soka nchini.

Mabao mengine katika mechi hiyo yalifungwa na Mzimbabwe Prince Dube, Pascal Msindo na Alassane Diao.

Akiwa nje ya eneo la hatari, Fei Toto aliachia kombora kali lililokwenda moja kwa moja wavuni na kumwacha kipa wa Kagera Sugar, Ramadhani Chalamanda, akiruka bila mafanikio.

Hata hivyo, mchezaji huyo aliyejiunga na Azam akitokea Yanga mwanzoni mwa msimu, amesema hashindani na mtu na hata kama atachukua kiatu cha dhahabu kwa kutwaa tuzo ya Mfungaji Bora, basi si kwa sababu alishindana na mchezaji mwingine.

Fei Toto alisema ataendelea kujituma katika kila mechi kwa kufunga mabao ili kuisaidia timu yake ifikie malengo.

Aliongeza siri ya kufanya vizuri ni kujituma katika mazoezi na kufuata maelekezo ya makocha wake ambao wanahitaji kuona msimu huu wanakuwa na matokeo bora zaidi.

„Mimi malengo yangu ni kupambania timu yangu na si kitu kingine, mengine yatajulikana huko huko mbele ya safari," alisema Fei Toto.

Msimu huu kumekuwa na mageuzi katika orodha ya wafungaji, kwani viungo washambuliaji wameonekana na kuchachamaa na kuingia katika vita ya kuwania kiatu cha dhahabu dhidi ya mastraika.

Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Maxi Nzengeli mwenye mabao saba anafuatia katika orodha hiyo akilingana na straika wa Simba, Jean Baleke wakati mshambuliaji, Waziri Junior wa KMC akiwa na magoli sita.

Dube ana mabao matano sawa na straika wa Singida Fountain Gate, Marouf Tchakei huku viungo washambuliaji, Kipre Junior wa Azam na Pacome Zouzoua wa Yanga, wote wakiwa na mabao manne kila mmoja.

Wakati huo huo, Bodi ya Ligi Nchini (TPLB), imeahirisha mechi saba za Ligi Kuu Tanzania Bara ili kupisha maandalizi ya mechi ya

INAENDELEA UK. 23

## Simba na Yanga majaribuni Bara

**Saada Akida na Faustine Feliciane, DODOMA**

BAADA ya kufanya vizuri katika michezo yao ya kimataifa, vigogo wa soka nchini wanarejea dimbani kusaka pointi muhimu katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba akiivaa KMC kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam huku Tabora United wakiikaribisha Yanga jijini, Dodoma.

Katika mechi ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara Simba iliichapa Kagera Sugar mabao 3-0 wakati Yanga iliifunga Mtibwa Sugar magoli 4-1.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo dhidi ya KMC yameenda vizuri na kila mmoja anatambua ugumu na umuhimu wa mechi hiyo.

Matola alisema wanafahamu wanahitaji kuvuna pointi tatu lakini pia wanatambua ubora wa wapinzani wao baada ya kuona mechi zao mbalimbali walizocheza, hivyo watawavaa kwa tahadhari na nidhamu ya hali ya juu ili kupata ushindi.

"Huu ni mchezo mpya kabisa, tuna kocha mpya na wao wana mwalimu mpya, hawajawahi kuonana, ninaimani utakuwa mchezo wa kiufundi na mbinu. Tutacheza kwa tahadhari kubwa. Tutacheza kwa umakini mkubwa kwa sababu ya timu hiyo ina wachezaji vijana ambao wanahitaji kucheza," alisema Matola.

Mwakilishi wa wachezaji, David Kameta, alisema wachezaji wote wako salama na tayari kwa mchezo huo ambao wanahitaji ushindi ili kufikia malengo ya kutwaa ubingwa mwisho wa msimu.

"Kwa sasa hatuna mechi ndogo kila timu tutakayokutana nayo tutacheza kwa ukubwa wake, kikubwa ni kusaka alama tatu muhimu, kesho (leo) ni mechi mpya na tunaingia na mbinu tofauti ili kupata ushindi bila kujali tutashinda kwa idadi ya mabao mangapi," alisema Kameta.

Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallin, alisema amefanyia kazi mapungufu ya kikosi chake na leo watapambana kusaka alama tatu

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002